na mine (kama katika mwili, sijui; kama inje ya mwili, sijui, Mungu anajua),
mutu huyu alichukuliwa juu hata mbingu ya tatu. 3 Nami ninajua mutu huyu
(kama katika mwili, kama inje ya mwili, sijui: Mungu anajua,) 4 ya kama ali-
chukuliwa juu hata Paradiso, akasikia maneno yasiyoweza kusemwa na yasi-
yofaa mutu kuyasema. 5 Kwa maneno ya mutu huyu nitajisifu, lakini kwa ajili
yangu, mimi sitajisifu, ila katika uzaifu wangu. 6 Maana kama ningetaka
kujisifu, singekuwa mupumbafu; kwa sababu nitasema kweli: lakini ninajizuiza,
ili mutu asinihesabie mimi zaidi ya hii anayoona kwangu, ao maneno anayosikia
kwa kinywa changu. 7 Na kwa sababu ya wengi wa mafunuo, kusudi nisijisifu
kupita kipimo, nilipewa mwiba katika mwili, mujumbe wa Shetani, anipige
mimi, nisijisifu kupita kipimo. 8 Kwa sababu ya kitu hiki nilisihi Bwana mara
tatu kinitoke. 9 Akaniambia: Neema yangu inafaa kwako: kwa sababu uwezo
wangu unakamilishwa katika uzaifu. Basi afazali sana nitajisifu katika uzaifu
wangu, uwezo wa Kristo ukae juu yangu. 10 Kwa sababu hii ninafurahi katika
uzaifu, katika matukano, katika mahitaji, katika mateso, katika taabu, kwa
ajili ya Kristo: maana wakati mimi ni zaifu, wakati ule ule nina nguvu. 11 Nime-
kuwa mupumbafu: ninyi mumenilazimisha mimi; maana ilinipasa kusifiwa na
ninyi; maana sikupungukiwa mitume walio wakubwa, hata kidogo, hata mimi
si kitu. 12 Kweli alama za mutume zilifanywa katikati yenu katika saburi yote,
kwa alama na maajabu na matendo ya uwezo. 13 Kwa maana ni kitu gani muli-
chopungukiwa kuliko makanisa mengine, ila kwa sababu mimi mwenyewe siku-
walemea ninyi? Munisamehe kosa hili.

Paulo anatafuta roho za watu, si mali zao

14 Tazama mara hii ni mara ya tatu mimi ni tayari kuja kwenu; wala sita-
walemea ninyi: kwani sitafuti vitu vyenu, lakini ninawatafuta ninyi; kwa sababu
haipasi watoto kuwekea wazazi akiba, lakini wazazi kwa watoto. 15 Kwa furaha
nyingi sana nitajitoa na tena nitatolewa kwa ajili ya roho zenu. Kama niki-
wapenda ninyi zaidi sana, ninapungukiwa kupendwa? 16 Lakini iwe hivi, mimi
sikuwalemea ninyi; lakini nikiwa na akili niliwapata ninyi kwa hila. 17 Nilipata
faida kwenu na mumoja wa watu niliowatuma kwenu? 18 Nilionya Tito, na
pamoja naye nilituma ndugu yule. Tito alipata faida kwenu? Hatukutembea kwa
Roho mumoja na katika nyayo zile zile?

19 Tena munazania ya kwamba tunajiuzuru kwenu? Tunasema mbele ya
Mungu katika Kristo. Lakini maneno yote, wapenzi, ni kwa ajili ya kuwajenga
ninyi. 20 Kwa sababu ninaogopa, hata wakati ninapokuja, sitawakuta ninyi
sawasawa ninavyotaka kuwakuta, na hata mimi nitaonekana kwenu si kama
munavyotaka kuniona; nisije nikakuta fitina, wivu, kasirani, ugomvi, masi-
ngizio, manongono, majivuno na makelele; 21 nami wakati nitakapokuja tena,
Mungu wangu ataninyenyekeza mimi mbele yenu, nikalilia wengi waliokosa
zamani, wala hawakutubu juu ya uchafu, na uasherati na tamaa mbaya waliyo-
yafanya.

Maonyo

13 Mara hii ni mara ya tatu ninakuja kwenu. Katika vinywa vya washu-
huda wawili ao watatu kila neno litasimamishwa. 2 Nimetangulia ku-
waambia ninyi, wakati nilipokuwa kwenu mara ya pili, na sasa nisipokuwa

12:4 Lk 23:43; Ufu 2:7. 12:5 2 Kor 11:30. 12:6 2 Kor 10:8; 11:16. 12:7 Yob 2:6. 12:10 Flp 4:13. 12:11 2 Kor 11:5. 12:12 Rom 15:19. 12:13 2 Kor 11:9. 12:14 2 Kor 13:1. 12:15 Flp 2:17. 12:18 2 Kor 8:6, 16–18. 12:20 2 Kor 10:2; 1 Kor 4:6. 12:21 2 Kor 2:1; 13:2. 13:1 Tor 19:15; Mt 18:16; 1 Tim 5:19.

kwenu, ninawaambia wazi wao waliotenda zambi mbele, na wengine wote, ya
kwamba, kama nikikuja tena sitawahurumia; 3 mukitafuta alama, kama ni
kweli Kristo anayesema ndani yangu. Yeye si zaifu kwenu, lakini ana uwezo
ndani yenu: 4 kwa sababu hata yeye alisulibiwa katika uzaifu, anaishi kwa nguvu
za Mungu. Kwa sababu sisi vilevile ni zaifu kama yeye, lakini tutaishi pamoja
kwa uwezo wa Mungu kwenu. 5 Mujitafute wenyewe kama ninyi ni katika
imani, mujijaribu wenyewe. Ninyi wenyewe hamujui ya kwamba Yesu Kristo
ni ndani yenu? kama musipokuwa mumekataliwa. 6 Lakini ninatumaini kama
mutajua ya kwamba sisi hatukukataliwa. 7 Lakini tunaomba Mungu musi-
fanye neno baya; si kwamba sisi tuonekane tumekubaliwa, lakini ninyi mufanye
maneno yaliyo mema, hata sisi tunaonekana kama tumekataliwa. 8 Kwani
hatuwezi kufanya neno juu ya kweli, lakini kwa ajili ya kweli. 9 Kwa maana
tunafurahi wakati sisi ni zaifu, na ninyi ni wenye nguvu: na tunaomba hili
vilevile, ukamilifu wenu. 10 Kwa hivi ninaandika maneno haya wakati nisi-
pokuwa kwenu, hata nikiwa kwenu, nisitumie ukali kwa kadiri ya amri nili-
yopewa na Bwana kwa kujenga, wala si kwa kubomoa.

Salamu

11 Mwisho, ndugu, kwa heri. Mukamilishwe; mufarijiwe; muwe na nia moja;
mukae katika salama; na Mungu wa mapendo na salama atakaa pamoja nanyi.
12 Musalimiane kwa busu takatifu. 13 Watakatifu wote wanawasalimu ninyi.
14 Neema ya Bwana Yesu Kristo, na mapendo ya Mungu, na ushirika wa Roho
Mutakatifu ukae pamoja nanyi wote.

BARUA YA PAULO MUTUME

KWA

WAGALATIA

Salamu ya Paulo

1 Paulo, Mutume (si wa watu, wala kwa mutu, ila kwa Yesu Kristo, na
Mungu Baba aliyemufufua toka wafu) 2 na ndugu zote walio pamoja nami,
kwa makanisa ya Galatia: 3 Neema iwe kwenu, na salama toka Mungu Baba,
na kwa Bwana wetu Yesu Kristo, 4 aliyejitoa kwa ajili ya zambi zetu, ili atuokoe
katika dunia hii mbovu ya sasa kama alivyopenda Mungu na Baba yetu, 5 awe
na utukufu milele na milele. Amina.

Habari nyingine

6 Ninastaajabu ya kuwa mumemwacha hivi upesi yeye aliyewaita ninyi katika
neema ya Kristo, mukageuka kwa Habari Njema ya namna nyingine, 7 isiyo
nyingine; lakini kuna watu wanaowataabisha ninyi, wakataka kugeuza Habari
Njema ya Kristo. 8 Lakini sisi, ama malaika ya mbinguni, tukiwahubiri ninyi
Habari Njema ya mbalimbali na ile tuliyowahubiri ninyi, alaaniwe. 9 Kama

13:4 4 Flp 2:7, 8. 13:5 1 Kor 11:28. 13:8 1 Kor 13:6. 13:10 2 Kor 2:3; 10:8, 11. 13:11 Flp 4:4; Rom 15:33. 13:12 1 Kor 16:20.

1:1 Gal 1:11, 12. 1:3 Rom 1:7. 1:4 Gal 2:20; 1 Tim 2:6; Tit 3:14; 1 Yn 5:19. 1:7 Mdo 15:1 24. 1:8 1 Kor 16:22.

tulivyosema kwanza, sasa tena ninasema mara ya pili. Mutu ye yote akiwahubiri ninyi Habari Njema ya mbalimbali na ile muliyopokea, alaaniwe. 10 Maana sasa ninashawishi watu ama Mungu? Ama ninataka kupendeza watu? Kwa sababu kama ningependeza watu, singekuwa mutumwa wa Kristo.

Habari Njema ya Paulo ilitoka kwa Mungu

11 Ninawajulisha ninyi ndugu zangu, Habari Njema iliyohubiriwa nami ya kuwa si ya namna ya watu. 12 Maana sikuipokea kwa mutu, wala sikufundishwa na mutu, lakini kwa ufunuo wa Yesu Kristo. 13 Maana mumesikia habari za matendo yangu zamani katika dini ya Wayuda, namna nilivyotesa zaidi kanisa la Mungu na kuliharibu; 14 nami nilitangulia katika dini ya Wayuda kuliko wengi walio wa wakati wangu katika kabila langu, nikizidi kuwa mwivu sana katika kushika hadizi za baba zangu. 15 Lakini Mungu, aliyenitenga katika tumbo la mama yangu; akaniita kwa neema yake, alipoona vema 16 kufunua Mwana wake ndani yangu, ili nihubiri habari zake katika Mataifa, mara moja sikufanya shauri pamoja na watu wenye mwili na damu, 17 wala sikupanda kwenda Yerusalema kwao waliokuwa mitume mbele yangu, lakini nilikwenda zangu katika Arabia, nikarudi tena Damasiki. 18 Kisha, nyuma ya miaka mitatu, nilipanda kwenda Yerusalema kuona Kefa, nikakaa kwake siku kumi na tano. 19 Lakini sikuona mitume wengine ila Yakobo, ndugu yake Bwana. 20 Na maneno ninayowaandikia ninyi, angalieni, mbele ya Mungu, sisemi uwongo. 21 Halafu nilikwenda pande za Suria na Kilikia. 22 Lakini sikujulikana uso wangu na makanisa ya Wayuda yaliyo katika Kristo; 23 lakini walisikia tu ya kwamba yeye aliyetutesa zamani, sasa anahubiri imani ile aliyoiharibisha zamani. 24 Wakatukuza Mungu kwa ajili yangu.

2 Halafu nyuma ya miaka kumi na mine, nilikwenda tena Yerusalema pamoja na Barnaba, nikachukua Tito pamoja nami. 2 Nami nilikwenda kwa ufunuo, nikawaelezea Habari Njema ile niliyohubiri katika Mataifa, lakini kwa siri kwao wenye heshima, isiwe hakose ninapiga mbio bule, ao nilipiga mbio bule. 3 Lakini Tito aliyekuwa pamoja nami, yeye aliyekuwa Muyunani, hakulazimishwa kutahiriwa 4 lakini kwa ajili ya ndugu za uwongo walioingizwa kwa siri. Hawa waliingia kwa siri wapate kupeleleza uhuru wetu tulio nao katika Yesu Kristo, watutie katika utumwa; 5 lakini hata saa moja hatukujitia chini yao, ili kweli ya Habari Njema ikae pamoja nanyi. 6 Lakini wale wenye sifa walionekana kama watu wakubwa (namna yao si kitu kwangu, Mungu hakubali uso wa mutu) ninasema hawa wenye sifa hawakuniongezea kitu. 7 Lakini mbali na maneno haya, walipoona ya kuwa niliwekwa kwa Habari Njema ya wasiotahiriwa, kama vile Petro alivyowekwa kwa Habari Njema ya waliotahiriwa; 8 maana yeye aliyewezesha Petro kwa utume wa waliotahiriwa, ndiye yeye aliyeniwezesha mimi kwenda Mataifa, 9 tena wakati walipokwisha kujua neema niliyopewa, Yakobo, na Kefa, na Yoane, waliohesabiwa kama nguzo, wakanipa mimi na Barnaba mukono wa kuume wa ushirika, ili sisi twende kwa Mataifa, na wao waende kwa watu wa tohara. 10 Ila neno moja walitutakia, tukumbuke masikini, na neno hili nilitaka sana kufanya.

11 Lakini wakati Petro alipokuja Antiokia, nilishindana naye, uso kwa uso,

1:10 1 Tes 2:4. 1:13 Mdo 26:4–20. 1:14 Mdo 22:3. 1:15 Rom 1:1; Yer 1:5; Isa 49:1. 1:16 Gal 2:7; Mt 16:17. 1:18 Mdo 9:26. 1:19 Mt 13:55. 1:21 Mdo 9:30.

2:1 Mdo 15:2. 2:2 Gal 6:9. 2:3 Mdo 16:3. 2:4 Mdo 15:1, 24. 2:5 Gal 3:1. 2:7 Mdo 9:15; 15:12; 22:21. 2:9 Yn 1:42. 2:10 Mdo 11:30; 12:25.

kwa sababu alistahili hukumu; 12 kwa sababu mbele ya kuja kwa watu wengine waliotoka kwa Yakobo, alikulaga pamoja na Mataifa, lakini walipofika, akarudi nyuma, akajitenga, akiwaogopa waliotahiriwa. 13 Na Wayuda waliobaki wakajigeuza pamoja naye, hata Barnaba alichukuliwa na kujigeuza kwao. 14 Lakini nilipoona mimi ya kuwa njia zao hazikwenda sawasawa na kweli ya Habari Njema, nilimwambia Petro mbele ya watu wote: Kama wewe, ukiwa Muyuda, unafuata desturi za Mataifa, wala si za Wayuda, kwa nini unashurutisha Mataifa kufuata desturi za Wayuda?

Haki kwa imani

15 Sisi tulio Wayuda kwa asili, wala si wenye zambi wa Mataifa, 16 tukijua kwamba mutu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria, lakini kwa imani ya Yesu Kristo; sisi tuliamini Yesu Kristo,ili tuhesabiwe haki kwa imani ya Kristo, wala si kwa matendo ya sheria; maana hapana mutu atakayehesabiwa haki kwa matendo ya sheria. 17 Lakini kama sisi wenyewe tulipokuwa tukitafuta kuhesabiwa haki katika Kristo, tulionekana wenye zambi, Ee, Kristo amekuwa mutumishi wa zambi? Hapana, hata kidogo. 18 Maana nikijenga tena maneno yale niliyoyabomoa, ninaonyesha ya kuwa mimi mwenyewe mukosaji. 19 Maana, kwa sheria, mimi nilikufa kwa sheria, nipate kuwa hai kwa Mungu.

Kristo anaishi ndani ya mwamini

20 Nimesulibiwa pamoja na Kristo, lakini ni hai; wala si mimi, lakini Kristo ni hai ndani yangu; na uzima nilio nao sasa katika mwili, ni uzima wa imani iliyo ya Mwana wa Mungu aliyenipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu. 21 Sibatili neema ya Mungu, maana ikiwa haki ilikuwa kwa sheria basi Kristo alikufa bule.

Roho Mutakatifu, zawadi ya imani

3 Ee! Wagalatia pasipo akili, ni nani aliyewaloga ninyi, musisadiki kweli, ninyi muliokuwa na Yesu Kristo, aliyewekwa mbele ya macho yenu ya kuwa amesulibiwa? 2 Ninataka kujua neno hili moja kwenu. Mulipokea Roho kwa matendo ya sheria, ao kwa kusikia kwa imani? 3 Ee, ninyi wajinga namna hii? Mukianza katika Roho, munataka mutimilizwe katika mwili? 4 Munateswa na maneno mengi hivi bule? Ikiwa ni bule kweli? 5 Basi yeye aliyewapa ninyi Roho, na kufanya matendo ya uwezo katikati yenu, anafanya hivi kwa matendo ya sheria ama kwa kusikia kwa imani?

Abrahamu ni baba ya waamini

6 Kama vile Abrahamu alivyoamini Mungu, akahesabiwa haki. 7 Jueni basi, wale walio wa imani, hawa ni watoto wa Abrahamu. 8 Na andiko likiona tangu zamani kwamba Mungu atahesabia haki Mataifa kwa imani, lilihubiri Abrahamu Habari Njema mbele, likisema: Kwa wewe Mataifa yote watabarikiwa. 9 Basi walio wa imani watabarikiwa pamoja na Abrahamu mwenye imani. 10 Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria ni chini ya laana, maana imeandikwa: Amelaaniwa kila mutu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati ayafanye. 11 Ni wazi ya kwamba hakuna mutu anaye-

2:12 Mdo 11:3. 2:16 Mdo 15:10, 11; Efe 2:8; Rom 3:20, 28; 4:5; 11:6; Zab 143:2. 2:19 Rom 7:6. 2:20 Yn 13:1; 17:23; 1 Yn 3:16; Gal 1:4.

3:6 Mwa 15:6. 3:8 Mwa 12:3; 18:18; Mdo 3:25. 3:9 Rom 4:16. 3:10 Tor 27:26. 3:11 Hab 2:4; Rom 1:17; Ebr 10:38.

hesabiwa haki kwa sheria katika macho ya Mungu; kwa sababu wenye haki
wataishi kwa imani. 12 Na torati si kwa imani, lakini mutu anayetenda maneno
haya ataishi kwa maneno haya.

Baraka kwa Mataifa kwa Kristo

13 Kristo alitukomboa kwa laana ya torati, akiwa alifanywa laana kwa ajili
yetu, kama ilivyoandikwa: Amelaaniwa kila mutu aliyetundikwa juu ya muti;
14 ili baraka ya Abrahamu ifikie Mataifa kwa Yesu Kristo; tupate kupokea ahadi
ya Roho kwa imani.

15 Ndugu zangu, ninasema kwa namna ya watu, hata agano la watu, likisibitika, mutu halibatili wala kuliongeza neno. 16 Lakini kwa Abrahamu ahadi
zilisemwa, na kwa uzao wake. Hasemi wazao kama wengi, ila kama mumoja,
muzao wako ndiye Kristo. 17 Ninasema maneno haya; agano lililosibitika
mbele na Mungu, torati iliyokuwa miaka mia ine na makumi tatu nyuma,
haiwezi kulibatili, hata kutangua ahadi. 18 Kwa maana uriti ukiwa kwa sheria,
sio tena kwa ahadi, lakini Abrahamu alipewa ahadi ya Mungu. 19 Torati ni nini
basi? Iliingizwa kwa sababu ya makosa hata muzao atakapokuja aliyepewa
ahadi; iliamriwa kwa malaika katika mukono wa mupatanishi. 20 Aliye mupatanishi si mupatanishi wa mumoja, lakini Mungu ni mumoja.

21 Basi torati haipatani na ahadi ya Mungu? Hapana hata kidogo. Maana
kama sheria ingalitolewa iliyoweza kufanya uzima, kweli haki ingalikuwa kwa
sheria. 22 Lakini maandiko yalifunga wote chini ya zambi, kusudi wenye kuamini wapewe ahadi kwa imani ya Yesu Kristo.

Kazi ya sheria

23 Lakini mbele ya kuja kwa imani, tulichungwa chini ya sheria, tumefungwa
kwa imani itakayofunuliwa nyuma. 24 Hivyo torati ilikuwa mwalimu wa kutuleta kwa Kristo, tupewe haki kwa imani. 25 Lakini sasa imani imekwisha kuja,
hatuko tena chini ya mwalimu; 26 maana ninyi wote ni wana wa Mungu, kwa
imani, katika Yesu Kristo. 27 Maana ninyi wote muliobatizwa na kuingizwa
katika Kristo, mumevaa Kristo. 28 Hapana Muyuda, wala Muyunani, hapana
mutumwa wala huru, hapana mwanamume wala mwanamuke. Maana ninyi
wote ni mumoja katika Yesu Kristo. 29 Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mumekuwa uzao wa Abrahamu na wariti kwa ahadi.

4 Lakini ninasema ya kuwa muriti, wakati alipokuwa mutoto, anaonekana
kama mutumwa hata akiwa bwana wa wote; 2 lakini ndiye chini ya wasimamishi na mawakili hata wakati uliokwisha kuamriwa na baba. 3 Vile na sisi,
tulipokuwa watoto, tulifungwa chini ya desturi za dunia; 4 lakini wakati ulipomalizwa, Mungu alituma Mwana wake, aliyezaliwa na mwanamuke, aliyezaliwa chini ya sheria 5 ili awakomboe waliokuwa chini ya sheria, tupate kupokea hali ya wana. 6 Lakini kwa sababu ninyi ni wana, Mungu alituma Roho
ya Mwana wake katika mioyo yetu, anayelia: Aba, Baba. 7 Basi, wewe si mutumwa tena, lakini mwana; na kama mwana, basi muriti wa Mungu kwa Kristo.
8 Lakini wakati ule musipojua Mungu, mumetumikia wao wasio miungu kwa

3:12 Law 18:5; Rom 10:5. 3:13 Rom 8:3; Tor 21:23; 2 Kor 5:21. 3:16 Mwa 12:7; 13:15; 17:7; 22:18; 24:7. 3:17 Kut 12:40. 3:18 Rom 11:6. 3:19 Rom 5:20; Ebr 2:2; Mdo 7:38, 53. 3:21 Rom 8:2–4. 3:22 Rom 3:9–19; 11:32. 3:23 Gal 4:3; 1 Pet 1:5. 3:25 Rom 10:4. 3:26 Yn 1:12; Rom 8:17. 3:27 Rom 6:3; 13:14. 3:28 Rom 10:12; 1 Kor 12:13. 3:29 Rom 9:7. 4:3 Gal 3:23; 5:1; Kol 2:20. 4:4 Efe 1:10. 4:5 Gal 3:13, 26. 4:6 Rom 8:15. 4:7 Gal 3:29; Rom 8:16, 17.

asili; 9 lakini sasa mukikwisha kujua Mungu, ama afazali mukijuliwa na Mungu,
sababu gani mumegeuka tena kwa maneno ya uzaifu na masikini, muliyotaka
muyatumikie tena? 10 Munashika siku, na miezi, na nyakati, na miaka.
11 Ninawaogopa ninyi, isiwe hakose ninajitaabisha kwenu bule.

Sheria na neema

12 Ninaomba kwenu, ndugu zangu, muwe kama mimi, kwa sababu mimi
kama ninyi. Hamukunitendea mabaya yo yote: 13 lakini munajua ya kuwa kwa
uzaifu wa mwili, niliwahubiri ninyi kwanza Habari Njema; 14 na jaribu lililokuwa katika mwili wangu hamukuzarau, wala hamukukataa, lakini mukanikaribisha kama malaika ya Mungu, kama Yesu Kristo. 15 Basi wapi furaha
yenu? Maana ninawashuhudia ninyi kwamba ingaliwezekana mungaliondosha
macho yenu, mukanipa mimi. 16 Basi nimekwisha kuwa adui yenu kwa sababu
ninawaambia ninyi yaliyo kweli? 17 Wao wanawatamani ninyi, lakini si kwa
wema; lakini wanataka kuwafunga ninyi inje, muwatafute wao. 18 Lakini ni
vizuri kutafuta sana neno jema siku zote, wala si wakati mimi ni pamoja nanyi
tu. 19 Watoto wangu wadogo, ninao tena uchungu kwa ajili yenu hata Kristo
atakapoonekana ndani yenu. 20 Ndivyo, ninataka kuwa pamoja nanyi sasa, na
kugeuza sauti yangu; kwa sababu ninaona shaka kwa ajili yenu.

21 Muniambie, ninyi munaotaka kuwa chini ya sheria, hamusikii sheria?
22 Kwa maana imeandikwa: Abrahamu alikuwa na wana wawili, mumoja kwa
kijakazi, na mumoja kwa huru. 23 Lakini yule wa kijakazi alizaliwa kwa mwili;
yule wa huru kwa ahadi. 24 Maneno haya ni mufano; kwa maana wanawake
hawa ni maagano mawili; moja toka mulima Sinai, lililozaa kwa utumwa, ndilo
Hagari. 25 Maana Hagari ni mulima Sinai ulio katika Arabia, umefanana na
Yerusalema wa sasa, naye katika utumwa pamoja na watoto wake. 26 Lakini
Yerusalema wa juu ni huru, ndiye mama yetu sisi sote. 27 Kwa maana imeandikwa:

> Furahi, tasa usiyezaa,
> Paza sauti, ukalie, wewe usiwe na uchungu.
> Kwa sababu watoto wake aliyeachwa ni wengi kuliko wake aliye na
> mume.

28 Sisi, ndugu zangu, kama Isaka, watoto wa ahadi; 29 lakini kama wakati ule
aliyezaliwa kwa mwili alitesa yule aliyezaliwa kwa Roho, vivyo na sasa. 30 Andiko linasema nini? Fukuza kijakazi na mwana wake, kwa maana mwana wa
kijakazi hatariti pamoja na mwana wa huru. 31 Basi, ndugu zangu, sisi si watoto
wa kijakazi, lakini wake aliye huru.

5 Kristo alitufanya huru kwa uhuru; basi, simameni, musiingie tena katika
kongwa la utumwa.

2 Angalieni, mimi Paulo ninawaambia ninyi ya kwamba, mukitahiriwa,
Kristo hatawafaidia ninyi neno. 3 Ninashuhudia tena kila mutu anayetahiriwa
ya kwamba imemupasa kufanya torati yote. 4 Mumetengwa na Kristo, ninyi
munaotaka kuhesabiwa haki kwa sheria; mumeanguka na kutoka katika
neema. 5 Maana sisi kwa Roho tunatazamia tumaini la haki kwa njia ya imani.
6 Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa;

4:10 Rom 14:5; Kol 2:16. 4:11 2 Yn 1:8. 4:12 2 Kor 2:5. 4:13 Mdo 16:6; 1 Kor 2:3. 4:14 Mdo 14:11, 12. 4:16 Amo 5:10. 4:17 Gal 1:7. 4:19 1 Kor 4:15. 4:21 Gal 3:23. 4:22 Mwa 16:15; 21:2, 9. 4:23 Rom 9:7–9; Mwa 17:16. 4:24 Gal 5:1; Rom 8:15. 4:26 Ebr 12:22. 4:27 Isa 54:1. 4:29 Mwa 21:9. 4:30 Mwa 21:10, 12; Yn 8:35. 4:31 Gal 3:29.

5:1 Gal 4:5, 31; Mdo 15:10. 5:2 2 Kor 10:1. 5:6 Gal 6:15; 1 Kor 7:19.

lakini imani inayotenda kazi kwa mapendo. 7 Mulikuwa mulikwenda mbio vizuri, ni nani aliyewazuiza ninyi, msitii kweli? 8 Kushawishi huku hakukutoka kwa yeye aliyewaita ninyi. 9 Chachu kidogo inachacha fungu nzima. 10 Nina matumaini kwenu katika Bwana, kwamba hamutakuwa na nia ya namna nyingine; lakini yeye anayewafazaisha ninyi, atachukua hukumu yake, kwake aliye. 11 Na mimi, ndugu zangu, nikihubiri habari za kutahiriwa, kwa nini ninateswa hata sasa? Hivyo kwazo la musalaba limeondoka. 12 Ninapenda ya kuwa watu hawa wanaowasumbua ninyi, wangejikata nafsi zao.

13 Maana, ndugu zangu, ninyi muliitwa mupate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kufuata mwili, lakini mutumikiane kwa mapendo. 14 Maana torati yote imetimia katika neno moja, nalo ni hili: Upende jirani yako kama nafsi yako. 15 Lakini mukiumana na kulana, angalieni musiangamizane.

Kushinda mwili kwa Roho Mutakatifu

16 Basi ninasema: Kwendeni kwa Roho, wala hamutatimiza tamaa za mwili. 17 Kwa sababu mwili unatamani ukishindana na Roho, na Roho anashindana na mwili; kwa maana hizi zinapigana, hata hamuwezi kufanya maneno yale munayotaka. 18 Lakini mukiongozwa na Roho, hamuko chini ya sheria. 19 Basi matendo ya mwili yanaonekana, ndiyo: uasherati, uchafu, uzini, 20 kuabudu sanamu, ulozi, uadui, ugomvi, uwivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, 21 husuda, uuaji wa mutu, ulevi, ulafi, na yanayofanana na maneno haya; juu ya maneno haya ninawaambia ninyi mbele kama nilivyowaambia ninyi zamani; watu wale wanaotenda maneno ya namna hii, hawatariti ufalme wa Mungu. 22 Lakini matunda ya Roho ni mapendo, furaha, salama, uvumilivu, neema, wema, uaminifu, 23 upole, ujizuiza, hakuna sheria juu ya maneno ya namna hii. 24 Nao walio watu wa Kristo wamesulibisha mwili pamoja na mawazo mabaya na tamaa mbaya. 25 Tukiishi kwa Roho, twende kwa Roho. 26 Tusijisifu bule, tukichokozana, tukitamanana.

Ndugu mwenye kukosa

6 Ndugu zangu, kama mutu akipatwa katika kosa lo lote, ninyi watu wa Roho, murudishe mutu huyu katika roho ya upole; ukijiangalia nafsi yako usijaribiwe wewe mwenyewe. 2 Muchukuliane mizigo yenu, vile mutatimiliza sheria ya Kristo. 3 Maana mutu akijizania kuwa kitu, naye si kitu, anajidanganya yeye mwenyewe. 4 Lakini kila mutu apime kazi yake mwenyewe, kisha atakuwa na sababu ya kujisifu yeye mwenyewe, si kwa watu wengine. 5 Kwa sababu kila mutu atachukua muzigo wake mwenyewe.

Kupanda na kuvuna

6 Lakini yeye aliyefundishwa katika neno, ashiriki naye aliyefundisha katika maneno yote yaliyo mema. 7 Musidanganywe: Mungu hazihakiwi; yo yote mutu anayopanda, ndiyo atakayovuna. 8 Maana yeye anayepanda kwa mwili wake mwenyewe, kwa mwili atavuna uharibifu; lakini yeye anayepanda kwa Roho, kwa Roho atavuna uzima wa milele. 9 Na katika kutenda mema, tusi-

5:8 Gal 1:6. 5:9 1 Kor 5:6. 5:10 Gal 1:7; 2 Kor 11:15. 5:11 1 Kor 1:23. 5:12 Zab 12:3. 5:13 1 Pet 2:16. 5:14 Law 19:18. 5:17 Rom 7:15, 23; Yak 4:5; 1 Pet 2:11. 5:18 Rom 8:14. 5:19 1 Kor 6:9, 10. 5:21 Efe 5:5; Ufu 22:15. 5:22 Efe 5:9. 5:23 1 Tim 1:9. 5:24 Rom 6:6; Kol 3:5; 1 Pet 2:11. 5:25 Rom 8:4. 5:26 Flp 2:3.

6:1 Mt 18:15; Yak 5:19. 6:4 2 Kor 13:5. 6:5 Rom 14:12. 6:6 1 Kor 9:14. 6:8 Rom 8:13; Yn 6:63; 3:6. 6:9 2 Tes 3:13.

choke; kwa maana kwa wakati wake tutavuna, tusipozimia. 10 Basi, tukiona nafasi, tutende mema kwa watu wote, zaidi kwao walio wa nyumba ya imani.

Mafundisho ya mwisho

11 Tazameni, kwa herufi kubwa gani nimewaandikia ninyi kwa mukono wangu mwenyewe. 12 Wote wanaotaka kuonekana kuwa wazuri kwa mwili, wanawalazimisha ninyi kutahiriwa; wasiteswe tu kwa ajili ya musalaba wa Kristo. 13 Nao waliotahiriwa hawashiki sheria; lakini wanataka ninyi kutahiriwa, wapate kujisifu kwa miili yenu. 14 Lakini mimi, nisijisifu hata kidogo juu ya kitu ila musalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo; kwa yeye dunia hii imesulibiwa kwangu, na mimi kwa dunia. 15 Kwa sababu kutahiriwa si kitu, wala kutokutahiriwa, lakini kiumbe kipya. 16 Na wote wanaofuata amri hii, salama kwao na rehema, na kwa Israeli wa Mungu.

17 Tangu sasa mutu asinisumbushe, kwa maana ninachukua katika mwili wangu chapa zake Yesu.

18 Ndugu zangu, neema ya Bwana wetu Yesu Kristo iwe pamoja na roho zenu. Amina.

BARUA YA PAULO MUTUME

KWA

WAEFESO

1 Paulo mutume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu, kwa watakatifu walio katika Efeso, na kwao wanaoamini Kristo Yesu: 2 Neema iwe kwenu na salama toka Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.

Baraka kubwa za Mungu

3 Abarikiwe Mungu na Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za roho katika pahali pa mbingu ndani ya Kristo; 4 kama vile alivyotuchagua ndani yake mbele ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, na pasipo kilema mbele yake katika mapendo. 5 Kwa kuwa alitangulia kutuchagua ili tufanywe wana wake kwa njia ya Yesu Kristo sawasawa ilivyopendeza mapenzi yake, 6 na kwa sifa ya utukufu wa neema yake aliyotupa sisi katika huyu Mupendwa. 7 Katika yeye tuna ukombozi wetu kwa njia ya damu yake, usamehe wa zambi zetu, sawasawa na wingi wa neema yake, 8 aliyozidisha kwetu katika hekima yote na akili, 9 akikwisha kutujulisha siri ya mapenzi yake, sawasawa ilivyomupendeza kukusudi ndani yake 10 hata madaraka ya kutimilika ya nyakati kujumlisha vitu vyote ndani ya Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani; katika yeye. 11 Na ndani yake sisi vile-vile tulifanywa uriti, tukichaguliwa tangu zamani sawasawa na kusudi lake anayefanya maneno yote kwa shauri la mapenzi yake; 12 ili tupate kuwa sifa ya utukufu wake, sisi tuliowekea Kristo tumaini letu mbele. 13 Ndani yake

6:10 2 Pet 1:7. 6:12 Gal 5:11; Flp 3:18. 6:14 1 Kor 1:31; 2:2. 6:15 Gal 5:6; 1 Kor 7:19. 6:16 Zab 125:5; 128:6; Flp 3:3. 6:17 2 Kor 4:10.

1:1 Rom 1:7; Kol 1:1; 1 Kor 1:2. 1:2 Kol 1:2. 1:3 Efe 2:6. 1:4 Yn 15:16; 17:24; Efe 5:27; Rom 8:29. 1:5 Yn 1:12. 1:6 Mt 3:17; Kol 1:13. 1:7 Kol 1:14, 20; Efe 2:7; 3:8, 16. 1:8 Kol 1:9. 1:9 Efe 3:9; Rom 16:25. 1:10 Gal 4:4; Kol 1:16. 1:11 Kol 1:12; Rom 8:28. 1:13 Efe 4:30; Kol 1:5, 6.

ninyi vilevile, wakati muliposikia neno la kweli, Habari Njema ya wokovu wenu,—ndani yake mumekwisha kuamini vilevile na kutiwa muhuri wa Roho Mutakatifu ya ahadi. [14] Ndiye aliye arabuni ya uriti wetu, ili kuleta ukombozi kwa mali yake mwenyewe, kuwa sifa ya utukufu wake.

Maombi

15 Kwa sababu hii mimi vilevile, nikikwisha kusikia habari za imani katika Bwana Yesu iliyo katikati yenu, na munayoonyeshea watakatifu wote, [16] siachi kuleta asante kwa ajili yenu, nikiwataja ninyi katika maombi yangu; [17] ili Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba ya utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumujua yeye; [18] macho ya mioyo yenu yatiwe nuru ili mujue tumaini la kuita kwake, na wingi wa utukufu wa uriti wake katika watakatifu, [19] na ukubwa wa kupita wa uwezo wake kwetu tunaoamini, kwa kadiri ya utendaji wa nguvu wa uwezo wake [20] aliotenda katika Kristo, wakati alipomufufua toka wafu, na kumukalisha kwa mukono wake wa kuume katika pahali pa mbingu, [21] juu sana kuliko utawala wote na mamlaka na nguvu na usultani, na kila jina linalotajwa, si katika ulimwengu huu tu, lakini vilevile katika ule utakaokuja; [22] na ameweka vitu vyote chini ya miguu yake, akamuweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa kanisa [23] lililo mwili wake, utimilifu wake anayetimiza vyote katika vyote.

Wokovu mukubwa

2 Nanyi mulikuwa wafu kwa sababu ya makosa yenu na zambi zenu, [2] mulizotembea ndani yao zamani kwa kufuata mwenendo wa ulimwengu huu, na kwa kufuata mufalme wa uwezo wa anga, roho yule anayetenda kazi sasa ndani ya wana wa kuasi; [3] katikati yao sisi sote tuliishi vilevile, katika tamaa za mwili wetu, tukifanya mapenzi ya mwili na ya nia, na tulikuwa kwa tabia wana wa kasirani, kama wale wengine. [4] Lakini Mungu, akiwa mwenye rehema nyingi, kwa mapendo yake makubwa aliyotupenda sisi, [5] hata wakati tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu, alitupatiza uzima pamoja na Kristo (mumeokolewa kwa neema), [6] na alitufufua pamoja naye na kutukalisha pamoja naye katika pahali pa mbingu, katika Kristo Yesu; [7] hata katika nyakati za kuja aonyeshe wingi wa kupita kiasi wa neema yake kwa wema wake kwetu katika Kristo Yesu; [8] kwa maana mumeokolewa kwa neema kwa njia ya imani, wala neno hili halikutoka ndani yenu wenyewe, ni zawadi ya Mungu, [9] si kwa matendo, asiwe mutu atakayejisifu. [10] Maana sisi ni kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu ili tutende matendo mema Mungu aliyoyatengeneza mbele ili tutembee ndani yao.

Mwokozi mukubwa

11 Kwa ajili ya maneno haya mukumbuke ya kwamba zamani ninyi, watu wa Mataifa kwa maneno ya mwili, munaoitwa Wasiotahiriwa na wale wanaoitwa Waliotahiriwa, tohara katika mwili iliyofanyika kwa mikono; [12] kwamba kwa wakati ule mulikuwa mbali na Kristo, mumetengwa mbali na jamaa ya Israeli, na wageni kwa maagano ya ahadi. Mulikuwa hamuna tumaini wala Mungu

1:14 2 Kor 1:22; 5:5. 1:15 Kol 1:4, 9. 1:16 Kol 1:3. 1:17 Kol 1:10. 1:18 Tor 33:3, 4; Efe 12:27; Kol 1:5, 11. 1:19 2 Kor 13:4; Kol 1:11; 2:12. 1:20 Zab 110:1. 1:21 Kol 1:16; 2:10. 1:22 Zab 8:6; Mt 28:18; Efe 4:15; Kol 1:18. 1:23 Rom 12:5; Kol 1:19; 1 Kor 12:27; Efe 4:10.

2:1 Kol 1:21; 2:13. 2:2 Efe 6:12; Tit 3:3; Yn 12:31; Kol 1:13. 2:3 Kol 3:6. 2:5 Lk 15:24, 32; Efe 5:14; Rom 6:13. 2:6 Rom 8:10; Flp 3:20. 2:7 Efe 1:7. 2:8 Gal 2:16. 2:9 1 Kor 1:29. 2:10 Tit 2:14. 2:11 Efe 5:8. 2:12 Rom 9:4; 1 Tes 4:13.

duniani. [13] Lakini sasa, katika Kristo Yesu, ninyi muliokuwa mbali zamani mumekuwa karibu kwa damu ya Kristo. [14] Kwa maana yeye ni salama yetu, aliyetufanya sisi sote tuliokuwa wawili kuwa mumoja, na alibomoa kiambaza cha kati kilichotutenga. [15] Naye akikwisha kuondosha uadui katika mwili wake, ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo; ili apate kufanya hawa wawili kuwa mutu mupya mumoja ndani yake, akafanya salama. [16] Akapatanisha wote wawili na Mungu katika mwili mumoja, kwa njia ya musalaba wake, akikwisha kuua ule uadui kwa njia yake. [17] Akakuja na kuhubiri salama kwenu muliokuwa mbali, na salama kwao waliokuwa karibu. [18] Kwa maana kwa yeye sisi sote tumepata njia ya kukaribia Baba katika Roho mumoja. [19] Basi tangu sasa ninyi si wageni na wasafiri tena, lakini wenyeji pamoja na watakatifu, na watu wa nyumba ya Mungu. [20] Mumejengwa juu ya musingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kubwa la pembeni. [21] Katika yeye jengo zima linaunganishwa vizuri na kukua hata lipate kuwa hekalu takatifu katika Bwana. [22] Katika yeye ninyi vilevile munajengwa pamoja kuwa kao la Mungu katika Roho.

Ufunuo wa siri ya Mungu

3 Kwa sababu hii mimi Paulo, mufungwa wa Kristo Yesu kwa ajili yenu ninyi Mataifa, [2] ikiwa mumesikia habari za uwakili wa neema ile ya Mungu niliyopewa kwa ajili yenu; [3] ya kwamba kwa ufunuo nilijulishwa siri hii, kama nilivyoandika mbele kwa maneno machache. [4] Kwa maneno haya, wakati munaposoma munaweza kutambua ufahamu wangu katika siri ya Kristo. [5] Siri hii haikujulishwa kwa wana wa watu katika vizazi vingine, kama ilivyofunuliwa sasa kwa mitume yake watakatifu na manabii katika Roho; [6] ya kwamba Mataifa ni wariti pamoja nasi wa uriti mumoja, na wa mwili mumoja, na washiriki pamoja nasi wa ahadi hii katika Kristo Yesu kwa njia ya Habari Njema. [7] Nilifanywa muhubiri wa Habari Njema hii, kwa kadiri ya zawadi ya neema ile ya Mungu niliyopewa kwa kadiri ya utendaji wa uwezo wake. [8] Mimi, niliye mudogo kuliko yeye aliye mudogo wa watakatifu wote nilipewa neema hii ya kuhubiri Mataifa utajiri wa Kristo usiotafutikana; [9] na kuangaza watu wote wajue habari za madaraka ya siri iliyofichwa tangu zamani ndani ya Mungu aliyeumba vitu vyote; [10] ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulishwe na falme na mamlaka katika pahali pa mbingu; [11] kwa kadiri ya kusudi la milele alilokusudi katika Kristo Yesu Bwana wetu. [12] Katika yeye tuna uhodari na uwezo wa kukaribia katika tumaini kwa njia ya kumwamini. [13] Kwa hivi basi ninaomba musichoke kwa sababu ya mateso yangu kwa ajili yenu, yaliyo utukufu kwenu.

Maombi kwa kanisa

14 Kwa sababu ya neno hili ninapiga magoti yangu mbele ya Baba, [15] katika yeye jamaa zote mbinguni na duniani wanaitwa, [16] awape ninyi, kwa kadiri ya utajiri wa utukufu wake, kupata nguvu na uwezo kwa njia ya Roho yake katika mutu wa ndani; [17] hata Kristo akae ndani ya mioyo yenu kwa imani;

2:13 Isa 57:19; 52:7; Kol 1:20. 2:14 Isa 9:5; Gal 3:28; Kol 2:14. 2:15 2 Kor 5:17. 2:16 Kol 1:20, 22. 2:17 Isa 57:19; Zek 9:10. 2:18 Efe 3:12. 2:19 Efe 3:6; Ebr 12:22, 23. 2:20 Mt 16:18; Isa 28:16. 2:21 Kol 2:19. 2:22 1 Pet 2:5.

3:1 Flp 1:7, 13; Kol 1:24. 3:2 Kol 1:25. 3:3 Efe 1:9, 10; Kol 1:26. 3:6 Efe 2:13, 18, 19. 3:7 Kol 1:25, 29. 3:8 1 Kor 15:9, 10; Efe 1:7; Gal 1:16. 3:9 Rom 16:25; Kol 1:26, 27. 3:10 1 Pet 1:12; Rom 11:33; Kol 1:26. 3:11 Efe 1:11. 3:12 Yn 14:6; Ebr 4:16; Rom 5:2. 3:13 Kol 1:24. 3:16 Efe 1:7; 6:10; Kol 1:11. 3:17 Yn 14:23; Kol 1:23; 2:7.

mukiwa na shina na musingi katika mapendo, 18 ili mupate kufahamu pamoja
na watakatifu wote upana na urefu, na urefu juu na urefu chini, 19 na kujua
mapendo ya Kristo yanayopita ufahamu, mupate kutimizwa kwa utimilifu wote
wa Mungu.

Uwezo wa Mungu

20 Basi kwake yeye anayeweza kufanya mambo kuliko yote tunayoomba ao
kufikili, kwa kadiri ya uwezo unaotenda kazi ndani yetu, 21 kwake uwe utukufu
katika kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote kwa milele na milele.
Amina.

Umoja wetu

4 Kwa hivi basi mimi, mufungwa katika Bwana, ninawasihi ninyi mutembee
kama inavyostahili mwito mulioitwa, 2 kwa unyenyekevu wote na upole,
kwa uvumilivu, mukichukuliana katika mapendo; 3 mukiangalia sana kuchu-
nga umoja wa Roho katika kifungo cha salama. 4 Mwili ni mumoja, na Roho
mumoja kama vilevile mulivyoitwa katika tumaini moja la mwito wenu; 5 Bwana
mumoja, imani moja, ubatizo mumoja, 6 Mungu mumoja, naye ni Baba ya
wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote. 7 Lakini kila mutu kati-
kati yetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha zawadi ya Kristo. 8 Kwa hivi
anasema:

Wakati alipopanda juu, alifunga kifungo,
Akawapa watu zawadi.

9 (Basi neno hili: Alipanda, maana yake nini kama si kusema kwamba yeye
alishuka vilevile mupaka pande za chini za inchi? 10 Yeye aliyeshuka ndiye
aliyepanda vilevile juu sana kupita mbingu zote ili ajaze vitu vyote.) 11 Naye
alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wa-
hubiri wa Habari Njema; na wengine kuwa wachungaji na walimu; 12 kwa kusudi
la kukamilisha watakatifu, kwa kazi ya utumishi hata mwili wa Kristo uje-
ngwe; 13 hata sisi sote tufikie umoja wa imani, na kujua sana Mwana wa Mungu,
hata kuwa mutu muzima, hata kufika kipimo cha urefu wa utimilifu wa Kristo;
14 hata tusiwe tena watoto, tukitupwa huku na huku na kuchukuliwa kwa kila
upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, kwa udanganyifu mubaya;
15 lakini tukisema kweli katika mapendo tupate kukua katika maneno yote
ndani yake aliye kichwa, ndiye Kristo. 16 Katika yeye mwili wote ukiunganishwa
na kushikanishwa kwa kusaidia kwa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa
kila sehemu moja moja, unaongeza mwili upate kujijenga wenyewe katika ma-
pendo.

Mutu wa zamani na mutu mupya

17 Basi ninasema neno hili na kushuhudu katika Bwana hata musitembee
tena kama Mataifa wanavyotembea, katika ubatili wa nia zao, 18 ufahamu wao
uliotiwa giza, waliotengwa mbali na uzima wa Mungu kwa sababu ya ujinga
ulio ndani yao, sababu ya ugumu wa moyo wao; 19 waliokwisha kufa na kujitia
wenyewe katika mambo ya uasherati, kutenda uchafu wote kwa choyo. 20 La-
kini ninyi hamukujifundisha Kristo hivi; 21 ikiwa mulimusikia na kufundishiwa

3:18 Kol 2:2. 3:19 Kol 2:3. 3:20 Ko 1:29.

4:1 Kol 1:10. 4:2 Kol 3:12. 4:3 Kol 3:14, 15. 4:4 Rom 12:5. 4:5 Yn 10:16; 1 Kor 8:6. 4:6 1 Kor 12:6. 4:7 Rom 12:3, 6; 1 Kor 12:11. 4:8 Zab 68:18; Kol 2:15. 4:9 Yn 3:13. 4:11 1 Kor 12:28; Mdo 21:8. 4:12 1 Pet 2:5; 2 Tim 3:17. 4:13 Kol 1:28. 4:14 1 Kor 14:20; Ebr 13:9. 4:15 Efe 1:22; 5:23; Kol 1:18. 4:16 Kol 2:19. 4:17 Rom 1:21; Kol 2:4, 6. 4:18 Efe 2:12; Kol 1:21; 1 Pet 1:14. 4:19 Kol 3:5.

katika yeye, kama kweli ilivyo katika Yesu, 22 mwondoshe, kwa maneno ya
mwenendo wenu wa mbele, yule mutu wa zamani, anayeharibika kwa kufuata
tamaa za udanganyifu; 23 na mufanywe wapya katika roho ya nia zenu; 24 na
kuvaa yule mutu mupya aliyeumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na
utakatifu wa kweli.

Uzima mupya unabadilisha mutu

25 Kwa hivi, mukiondosha uwongo, museme kweli kila mutu na jirani yake;
kwa maana sisi ni viungo, kila mumoja kiungo cha mwenzake. 26 Mukasirike
na musifanye zambi; jua lisishuke na uchungu wenu haujakwisha bado; 27 wala
musimupe Shetani nafasi. 28 Yeye aliyeiba asiibe tena; lakini zaidi atumike aki-
fanya kazi njema kwa mikono yake, awe na kitu cha kugawia mwenye kuhitaji.
29 Masemo maovu yasitoke vinywani mwenu, lakini yaliyo mema kwa kujenga
kama inavyohitajiwa, yawape neema wale wanaosikia. 30 Wala musihuzunishe
Roho Mutakatifu ya Mungu, ndani yake mulitiwa muhuri hata siku ya uko-
mbozi. 31 Uchungu wote na hasira na kasirani na kelele na matukano yaondo-
shwe kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; 32 na mwonyeshe mema ninyi
kwa ninyi, muwe wenye huruma, mukisameheana, kama Mungu katika Kristo
alivyowasamehe ninyi.

Mwenendo mupya

5 Basi mufuate Mungu kama watoto wanaopendwa; 2 na mutembee katika
mapendo, kama Kristo vilevile alivyowapenda ninyi na kujitoa mwenyewe
kwa ajili yetu, toleo na zabihu kwa Mungu, kuwa harufu ya manukato. 3 Lakini
uasherati usitajwe katikati yenu, wala uchafu wo wote wala kutamani, kama
inavyostahili watakatifu; 4 wala aibu wala masemo yasiyo na maana, wala
maneno ya kuchekesha yasiyofaa; lakini zaidi maneno ya kushukuru. 5 Maana
munajua kabisa, ya kwamba hakuna mwasherati wala mutu muchafu wala
mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, ana uriti katika ufalme wa Kristo na
Mungu. 6 Mutu asiwadanganye ninyi na maneno bule; kwa kuwa kwa sababu
ya maneno haya kasirani ya Mungu inakuja juu ya wana wa kuasi. 7 Basi
musishirikiane pamoja nao; 8 kwa maana zamani mulikuwa giza, lakini sasa
mumekuwa nuru katika Bwana; mutembee kama watoto wa nuru. 9 (kwa
kuwa tunda la nuru ni katika wema wote na haki na kweli), 10 mukijaribu nini
inayopendeza Bwana. 11 Wala musishirikiane na matendo ya giza yasiyozaa
matunda, lakini zaidi muyahamakie; 12 kwa maana ni haya kusema juu ya
maneno wanayoyafanya kwa siri. 13 Lakini maneno yote wakati yanapohama-
kiwa, yanaonyeshwa na nuru; maana kila kitu kinachoonyeshwa ni nuru.
14 Kwa hivi anasema: Amka, wewe unayelala, na ufufuke katika wafu, na
Kristo atakuangaza.

Maonyo

15 Basi mwangalie sana namna munavyotembea, si kama watu wasio na
hekima, lakini kama watu wenye hekima; 16 mukikomboa wakati kwa sababu

4:22 Rom 8:13; Kol 3:9; Gal 6:8. 4:23 Rom 12:2. 4:24 Mwa 1:26. 4:25 Zek 8:16; Kol 3:8. 4:26 Zab 4:4; Yak 1:19, 20. 4:28 1 Tes 4:11. 4:29 Efe 5:4; Kol 3:16, 17; 4:6. 4:30 Efe 1:13; Isa 63:10. 4:31 Kol 5:8. 4:32 Mt 6:14; 18:22–35; Kol 3:12, 13.

5:1 Mt 5:48; Kol 3:12. 5:2 Gal 2:20; Ebr 10:10; Kol 3:13; Zab 40:6; Kut 29:18; Eze 20:41. 5:3 Efe 4:19; Kol 3:5. 5:4 Efe 4:29; Kol 3:8. 5:5 1 Kor 6:9, 10; Kol 3:5; Mdo 8:21. 5:6 Rom 1:18; Kol 2:4, 8. 5:8 Efe 2:11, 13; Lk 16:8; 1 Pet 2:9; Yn 12:36. 5:10 Rom 12:2. 5:11 Yn 16:8. 5:12 Rom 1:24. 5:13 Yn 3:20, 21. 5:14 Isa 26:19; 60:1; Rom 13:11; 6:13. 5:15 Mt 10:16; Kol 4:5

siku hizi ni za uovu. 17 Kwa hivi musiwe wajinga, lakini wenye kufahamu mapenzi ya Bwana. 18 Wala musilewe kwa mvinyo, ndani yake ni makelele, lakini mujazwe Roho; 19 mukisemezana ninyi kwa ninyi kwa zaburi na tenzi na nyimbo za roho, mukiimba na kushangilia Bwana mioyoni mwenu; 20 mukishukuru Mungu ndiye Baba siku zote kwa mambo yote, katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo; 21 mukinyenyekeana katika woga wa Kristo.

Hali ya mume na muke

22 Ninyi wake, mutii waume wenu, kama kutii Bwana. 23 Kwa maana mume ni kichwa cha muke, kama Kristo vilevile ni kichwa cha kanisa, naye ni Mwokozi wa mwili. 24 Lakini kama vile kanisa linavyotii Kristo, hivi vilevile wake watii waume wao katika kila kitu. 25 Waume, mupende wake wenu, kama vile Kristo alivyopenda kanisa, na kujitoa mwenyewe kwa ajili yake; 26 apate kulitakasa, akiwa amelisafisha kwa maji katika neno, 27 apate kulijiletea mwenyewe, kanisa la utukufu, pasipo alama wala kikunjo wala kitu cho chote kama hivi; lakini liwe takatifu na pasipo kilema. 28 Hivi vilevile inafaa waume kupenda wake wao wenyewe kama miili yao wenyewe. Yeye anayependa muke wake mwenyewe anajipenda mwenyewe. 29 Maana hakuna mutu aliyechukia mwili wake mwenyewe wakati wo wote; lakini anaukulisha na kuuchunga, kama Kristo vilevile anavyotendea kanisa. 30 Kwa kuwa sisi ni viungo vya mwili wake. 31 Kwa sababu ya neno hili mume ataacha baba yake na mama yake, na atafungana na muke wake, nao wawili watakuwa mwili mumoja. 32 Siri hii ni kubwa; lakini ninasema habari za Kristo na kanisa. 33 Lakini kila mutu apende muke wake mwenyewe kama nafsi yake mwenyewe; na muke asikose kuheshimu mume wake.

Watoto na wazazi

6 Watoto, mutii wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki. 2 Heshimu baba yako na mama yako (hii ni amri ya kwanza yenye ahadi) 3 upate heri, na uishi siku nyingi katika dunia. 4 Nanyi baba, musichokoze watoto wenu; lakini muwalee katika azabu na maonyo ya Bwana.

Watumishi na bwana zao

5 Watumwa, mutii wao walio bwana zenu kwa maneno ya mwili, kwa woga na kutetemeka, kwa roho moja, kama kutii Kristo; 6 si kwa utumwa wa macho tu, kama wenye kupendeza watu; lakini kama watumwa wa Kristo, mukifanya mapenzi ya Mungu kwa moyo; 7 kwa nia njema kama kutumikia Bwana, wala si watu; 8 mukijua ya kuwa kila neno jema mutu analotenda, atalipata tena toka Bwana, kama yeye ni mutumwa ao kama ni huru. 9 Na ninyi bwana, muwatendee hivi vilevile, mukiacha kuwaogopesha; mukijua ya kuwa yeye aliye Bwana wao na wenu ni mbinguni wala kwake hakuna upendeleo.

Askari ya Yesu na silaha zake

10 Basi kwa kumaliza, muzidi kuwa hodari katika Bwana, na katika uwezo wa nguvu zake. 11 Vaeni silaha zote za Mungu, mupate kuweza kusimama juu

5:17 Rom 12:2. 5:18 Mez 23:31; Lk 21:34. 5:19 Kol 3:16; Zab 33:2, 3. 5:20 Kol 3:17. 5:21 1 Pet 5:5. 5:22 Mwa 3:16; Kol 3:18; 1 Pet 3:1. 5:23 1 Kor 11:3; Kol 1:18. 5:25 Kol 3:19. 5:26 Tit 3:5. 5:27 Zab 45:13; 2 Kor 11:2. 5:30 Efe 1:23; 1 Kor 6:15; Mwa 2:23. 5:31 Mwa 2:24. 5:32 Ufu 19:7.

6:1 Kol 3:20. 6:2 Kut 20:12. 6:3 Tor 5:16. 6:4 Kol 3:21; Isa 50:5; Mez 2:2; 3:11; 19:18; Tor 6:7, 20–25; Zab 78:4. 6:5 Kol 3:22–25; Tit 2:9, 10; 1 Pet 2:18. 6:8 2 Kor 5:10. 6:9 Kol 4:1; 2 Sik 19:7; Mdo 10:34. 6:10 1 Kor 16:13; 1 Yn 2:14. 6:11 Efe 4:14; 2 Kor 10:4.

ya hila za Shetani. 12 Kwa maana kushindana kwetu si juu ya damu na nyama, lakini juu ya falme na mamlaka, juu ya watawala wa ulimwengu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika pahali pa mbingu. 13 Kwa hivi twaeni silaha zote za Mungu, mupate kuweza kushindana katika siku ya uovu, na mukikwisha kutimiza yote, kusimama. 14 Simameni basi, mumejifungia kweli viunoni, na kuvaa silaha ya haki kwa kifua, 15 na mumefunga miguu yenu na utayari wa Habari Njema ya salama; 16 zaidi ya yote mukitwaa ngabo ya imani, nayo mutaweza kuzima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. 17 Na pokeeni kofia ya wokovu, na upanga wa Roho, ndio Neno la Mungu; 18 kwa maombi yote na kusihi mukiomba kwa kila wakati katika Roho, na mukiangalia kwa neno hili na kudumu katika kuomba kwa ajili ya watakatifu wote, 19 na kwa ajili yangu, nipewe usemi kwa kufungua kinywa changu, ili nihubiri kwa uhodari siri ya Habari Njema, 20 kwa sababu yake mimi ni mujumbe katika minyororo; ili niseme kwa uhodari kama inavyofaa mimi kusema.

Kuagana

21 Lakini ili mupate kujua habari zangu vilevile, na hali yangu, Tikiko, ndugu mupendwa na mutumishi mwaminifu katika Bwana atawajulisha ninyi maneno yote; 22 niliyemutuma kwenu kwa kusudi hili tu, mupate kujua habari zetu, na apate kufariji mioyo yenu.

23 Salama iwe kwa ndugu, na mapendo pamoja na imani, toka Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo. 24 Neema iwe pamoja nao wote wanaopenda Bwana wetu Yesu Kristo katika mapendo yasiyokoma.

BARUA YA PAULO MUTUME

KWA

WAFILIPI

1 Paulo na Timoteo, watumwa wa Kristo Yesu, kwa watakatifu wote katika Kristo Yesu walio katika Filipi, pamoja na waangalizi na watumishi: 2 Neema iwe kwenu na salama toka Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo.

Paulo anawaombea

3 Ninashukuru Mungu wangu kila mara ninapowakumbuka ninyi, 4 siku zote katika maombi yangu yote kwa ajili yenu nikiomba kwa furaha, 5 kwa sababu ya ushirika wenu katika kuendesha Habari Njema toka siku ya kwanza hata sasa. 6 Na ninajua neno hili kabisa ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema ndani yenu ataitimiza hata siku ya Yesu Kristo; 7 kama vilevile ni haki nifikili maneno haya juu yenu wote, kwa sababu ninyi ni moyoni mwangu, kwa kuwa katika vifungo vyangu na katika kazi ya kulinda na kusimamia Habari Njema, ninyi ni washiriki pamoja nami katika neema hii. 8 Maana Mungu ni mushuhuda

6:12 Efe 2:2; Yn 14:30; Kol 1:13; 1 Pet 5:8, 9. 6:13 1 Fal 20:11. 6:14 Isa 11:5; 59:17; Lk 12:35; 1 Pet 1:13; 1 Tes 5:8. 6:15 Isa 52:7; 40:3, 9. 6:16 1 Pet 5:9; 1 Yn 5:4. 6:17 1 Tes 5:8; Hos 6:5; Isa 11:4; 49:2; 51:16. 6:18 Mt 26:41; Kol 4:2, 3. 6:19 Kol 4:3; 2 Tes 3:1; Mdo 4:29. 6:20 2 Kor 5:20; Kol 4:4. 6:21 Mdo 20:4; Kol 4:7; 2 Tim 4:12. 6:22 Kol 4:7, 8. 6:24 1 Pet 1:8.

1:1 1 Kor 1:2; 1 Tim 3:1, 8. 1:2 Rom 1:7. 1:3 Rom 1:8; 1 Kor 1:4. 1:6 Flp 2:13; 1 Kor 1:6–8. 1:8 Rom 1:9; 2 Kor 1:23; 1 Tes 2:5.

wangu wa hamu yangu niliyo nayo kwa ajili yenu katika moyo wake Kristo Yesu. 9 Na hii ndiyo ninayoomba, hata mapendo yenu yazidi kuongezeka mengi sana katika hekima na ufahamu wote; 10 ili mupate kukubali maneno yaliyo mema; ili muwe na moyo safi, pasipo kosa, mupaka siku ya Kristo; 11 mukijazwa matunda ya haki yaliyo kwa njia ya Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu.

Kuhubiri Kristo

12 Lakini, ndugu zangu, ninataka mujue ya kuwa maneno yote yaliyonipata yametokea zaidi kwa kuendesha Habari Njema; 13 hata vifungo vyangu vimeonekana katika Kristo nyumbani nzima mwa askari, na kwa wengine wote pia. 14 Na wengi wa ndugu zetu katika Bwana wakipata matumaini kwa ajili ya vifungo vyangu, wamezidi sana kusubutu kusema Neno la Mungu pasipo woga. 15 Ndiyo wengine wanahubiri Kristo kwa sababu ya hasidi na fitina; na wengine kwa nia njema. 16 Hawa wanahubiri kwa mapendo wakijua ya kuwa nimewekwa ili nisimamie Habari Njema. 17 Lakini wale wanahubiri Kristo kwa fitina, wala si kwa moyo safi, wakizania kuniongezea mateso katika vifungo vyangu. 18 Basi nini? Lakini kwa njia zote, ao kwa hila ao kwa kweli, Kristo anahubiriwa; na kwa neno hili ninafurahi, ndiyo, na nitafurahi. 19 Maana ninajua ya kuwa neno hili litageuka kuwa wokovu wangu, kwa sababu ya maombi yenu na kwa kusaidia kwa Roho ya Yesu Kristo, 20 kama vile ninavyotazamia sana na kutumaini ili nisiwe na haya katika neno lo lote, lakini hata na uhodari wote, kama siku zote, sasa vilevile Kristo atukuzwe ndani ya mwili wangu, ikiwa kwa maisha yangu ao ikiwa kwa mauti yangu. 21 Kwa maana kwangu kuishi ni Kristo, na kufa ni faida. 22 Lakini ikiwa kama kuishi katika mwili,—haya ni matunda ya kazi yangu, sijui nitakalolichagua. 23 Lakini ninasongwa katika mambo mawili, nikitamani kwenda zangu nikae pamoja na Kristo; maana ni vizuri zaidi sana; 24 lakini kudumu katika mwili kunahitajiwa zaidi kwa ajili yenu. 25 Na nikitumaini neno hili, ninajua ya kuwa nitakaa, ndiyo na kukaa pamoja nanyi wote, ili mupate kuendelea na kufurahi katika imani; 26 hata muzidi kujisifu kwenu katika Kristo Yesu juu yangu kwa sababu ya kuwa kwangu pamoja nanyi tena. 27 Lakini mwenendo wenu uwe kama inavyopasa Habari Njema ya Kristo, ili, nikikuja na kuwaona ninyi, ao nisipokuwa nisikie habari zenu ya kama munasimama imara katika roho moja, kwa moyo mumoja mukishindana kwa imani ya Habari Njema; 28 wala hamwogopi adui zenu katika neno lo lote; kwao neno hili ni alama wazi ya kupotea, lakini kwenu ni alama ya wokovu, unaotoka kwa Mungu. 29 Maana ninyi mumepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, lakini kuteswa vilevile kwa ajili yake; 30 mukiwa na mashindano yale yale muliyoyaona kwangu, na kusikia kwamba niliyo nayo hata sasa.

Nia ya Kristo

2 Basi ikiwa faraja yo yote katika Kristo, yakiwa matulizo yo yote ya mapendo, ukiwa ushirika wo wote wa Roho, ikiwa huruma yo yote na rehema, 2 jalizeni furaha yangu, ili muwe na nia moja, wenye mapendo mamoja, wenye roho moja, mukiwa na nia moja. 3 Musitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno, lakini kwa unyenyekevu kila mutu ahesabu mwenzake muzuri

1:10 Rom 2:18; 12:2; 1 Tes 5:23; Ebr 5:14. 1:11 Efe 5:9; 1:6, 12, 14; Yn 15:8. 1:12 2 Tim 2:9. 1:13 Flp 4:22; Efe 3:1. 1:18 Flp 2:17, 18. 1:19 Yob 13:16; 2 Kor 1:11. 1:20 1 Pet 4:16. 1:21 Gal 2:20. 1:22 Rom 1:13. 1:23 1 Fal 19:4; 2 Kor 5:8. 1:27 Kol 1:10; Flp 4:3; 1 Tes 2:12. 1:30 Mdo 16:22.

2:3 Gal 5:26; Rom 12:10.

kuliko yeye mwenyewe. 4 Kila mutu katikati yenu asiangalie maneno yake mwenyewe, lakini kila mutu aangalie maneno ya wengine. 5 Muwe na nia hii ndani yenu iliyokuwa ndani ya Kristo Yesu vilevile; 6 ndiye aliyekuwa na namna ya Mungu, hakuona kuwa sawa na Mungu kuwa kitu kushikamana nacho, 7 lakini alijifanya mwenyewe kuwa hana utukufu, akitwaa namna ya mutumwa, akakuwa na mufano wa mutu; 8 na akionekana na sura ya mutu, alijinyenyekeza mwenyewe, akakuwa mwenye kutii hata mauti, ndiyo mauti ya musalaba. 9 Kwa hivi Mungu vilevile alimutukuza sana, na kumupa jina lililo juu ya kila jina; 10 hata kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni na vya duniani, na chini ya dunia, 11 na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba.

Mungu anatenda kazi ndani yenu

12 Basi, wapendwa wangu, kama vile mulivyotii siku zote, si wakati nilipokuwa pamoja nanyi tu, lakini sasa zaidi sana wakati nisipokuwa, timizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. 13 Maana ni Mungu anayetenda kazi ndani yenu, kutaka na kutenda, kwa kutimiza kusudi lake jema. 14 Fanyeni maneno yote pasipo manunguniko wala mashindano; 15 mupate kuwa wana wa Mungu wasio na laumu wala udanganyifu, pasipo kipaku katika kizazi cha jeuri na ubishi, katikati yao ninyi munaonekana kama taa katika ulimwengu, 16 mukishika neno la uzima; nipate sababu ya kujisifu katika siku ya Kristo, ya kuwa sikukimbia bule wala sikujitaabisha bule. 17 Ndiyo, na kama mimi nikimimiwa juu ya zabihu na utumishi wa imani yenu, ninafurahi, na kufurahi pamoja nanyi wote. 18 Na vivyo hivyo ninyi furahini, na kufurahi pamoja nami.

Timoteo na Epafrodito

19 Lakini ninatumaini katika Bwana Yesu kuwatumia ninyi Timoteo bado kidogo, nifarijiwe vilevile nikijua hali yenu. 20 Maana sina mutu mwingine mwenye nia moja nami atakayeangalia hali yenu kweli kweli. 21 Maana wao wote wanatafuta maneno yao wenyewe, si maneno ya Kristo. 22 Lakini munajua sifa yake, ya kuwa ametumika pamoja nami kwa Habari Njema kama mwana na baba yake. 23 Basi ninatumaini kutuma huyu mara moja wakati nitakapojua yatakayonipata. 24 Lakini ninaamini katika Bwana ya kuwa nitakuja mimi mwenyewe vilevile bado kidogo. 25 Lakini niliona ni sharti kwangu kuwatumia ninyi Epafrodito, ndugu yangu na mutenda kazi pamoja nami, askari pamoja nami, na tena mutume wenu na mutumishi wa mahitaji yangu. 26 Kwa kuwa alikuwa na hamu sana kuwaona ninyi wote, akahuzunika sana kwa sababu mulisikia ya kama alikuwa na ugonjwa. 27 Kwa maana alikuwa na ugonjwa kweli kweli, karibu na kufa; lakini Mungu alimuhurumia; wala si yeye tu, lakini mimi vilevile, nisiwe na huzuni juu ya huzuni. 28 Kwa hivi nimefanya bidii nyingi zaidi kumutuma hata, wakati munapomwona tena, mupate kufurahi, nami nipunguziwe huzuni. 29 Mumupokee basi katika Bwana kwa furaha yote; na muheshimu watu kama huyu. 30 Maana kwa ajili ya kazi ya Kristo alikuwa karibu na kufa, akihatarisha uzima wake ili atimize yaliyokosa katika utumishi wenu kwangu.

2:4 1 Kor 10:24, 33. 2:6 Yn 1:1, 2; 17:5; Mwa 1:27; 3:5. 2:7 Isa 53:3; 2 Kor 8:9; Ebr 2:14, 17. 2:8 Ebr 12:2; 5:8; Yn 10:17. 2:9 Mdo 2:33; Efe 1:21; Ebr 1:3, 4. 2:10 Isa 45:23; Yn 5:23; Ufu 5:13. 2:12 1 Pet 1:17; Zab 2:11. 2:13 Yn 15:5; 2 Kor 3:5; 1 Tes 2:13. 2:14 1 Pet 4:9. 2:15 Mt 5:14; 10:16; Flp 1:10; Efe 5:8; Tor 32:5; Mdo 2:40. 2:16 1 Tes 2:19; Gal 2:2; Isa 49:4; 65:23. 2:17 Rom 15:16; 2 Tim 4:6. 2:18 Flp 3:1; 4:4. 2:20 1 Kor 16:10. 2:21 2 Tim 4:10, 16; Gal 4:17. 2:24 Flp 1:25. 2:25 Flp 4:18. 2:29 1 Kor 16:16; 1 Tim 5:17.

Angalieni adui za Kristo

3 Basi kwa kumaliza, ndugu zangu, furahini katika Bwana. Kuwaandikia
ninyi maneno haya hakunitaabishi, lakini kwenu ni faida. 2 Mujiangalie
kwa imbwa, mujiangalie kwa wale wanaotenda mabaya, mujiangalie kwa wale
wanaojikata wenyewe. 3 Maana sisi ni wale wa tohara tunaoabudu kwa Roho
ya Mungu, na kujisifu ndani ya Kristo Yesu, wala hatutumaini mwili. 4 Lakini
mimi ningeweza kutumaini mwili. Mutu ye yote akifikili kuwa na sababu ya
kutumaini mwili, mimi zaidi. 5 Nilitahiriwa siku ya nane, mimi ni mutu wa
Israeli, wa kabila la Benyamina, Muebrania wa Waebrania; kwa maneno ya
sheria, Mufarisayo; 6 kwa maneno ya bidii nikitesa kanisa; kwa maneno ya
haki iliyo katika sheria, pasipo kosa. 7 Lakini maneno yo yote yaliyokuwa faida
kwangu, niliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo. 8 Ndiyo kweli, na nina-
hesabu maneno yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri wa kujua Kristo Yesu
Bwana yangu; kwa ajili yake nimepata hasara ya maneno yote, nikiyahesabu
kuwa kama mavi ili nipate Kristo, 9 na nionekane ndani yake, nisiwe na haki
yangu mwenyewe inayopatikana kwa sheria, lakini ile inayopatikana kwa imani
katika Kristo, haki inayotoka kwa Mungu kwa njia ya imani; 10 ili nimujue
yeye, na uwezo wa ufufuko wake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa
na kufa kwake; 11 ili nipate kwa njia yo yote kufikia ufufuko toka wafu. 12 Si
kwamba nimekwisha kufika ao nimekwisha kukamilishwa; lakini ninakaza
mwendo ili nipate kushika neno lile kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo Yesu.
13 Ndugu zangu, sihesabu mimi kwamba nimekwisha kushika, lakini ninafanya
neno moja, nikisahau maneno yaliyo nyuma, na nikijinyosha kwa maneno
yaliyo mbele, 14 ninakaza mwendo hata nifikie mwisho wa zawabu ya mwito
mukubwa wa Mungu katika Kristo Yesu. 15 Basi sisi watimilifu, tuwe na nia
hii; na kama mukifikili maneno mengine katika neno lo lote, Mungu atawa-
funulia ninyi hili vilevile. 16 Lakini pahali tulipofika, tutembee kwa amri ile,
tukifikili neno moja.

Adui za musalaba wa Kristo

17 Ndugu zangu, munifuate na mutazame wao wanaotembea kwa kufuata
mufano tuliowapa ninyi. 18 Maana watu wengi wanatembea, juu yao nili-
waambia ninyi mara nyingi, na sasa ninawaambia ninyi hata kwa machozi, ya
kuwa wao ni adui za musalaba wa Kristo; 19 mwisho wao ni uharibifu, mungu
wao ni tumbo, utukufu wao ni haya yao, wanaofikili maneno ya dunia. 20 Kwa
maana sisi ni wenyeji wa mbingu; kutoka pale tunangoja Mwokozi, Bwana
Yesu Kristo; 21 atakayebadilisha mwili wetu wa haya upate kufanana na mwili
wake wa utukufu, kwa uwezo ule anaoweza kutiisha vitu vyote viwe chini yake.

Upatanisho

4 Kwa sababu hii, ndugu zangu, wapendwa wangu ninaowaona hamu sana,
furaha yangu na taji yangu, simameni imara katika Bwana, wapendwa
wangu.

2 Ninasihi Ewodia na Sintike wawe na nia moja katika Bwana. 3 Ndiyo,

3:1 Flp 2:18; 4:4. 3:2 Ufu 22:15. 3:3 Rom 2:29. 3:4 2 Kor 11:18, 22. 3:5 Mdo 26:5; Lk 1:59; 2:21. 3:7 Mt 13:44, 46. 3:9 Rom 3:21, 22. 3:10 Rom 6:3–5; 8:17; Gal 6:17. 3:11 Mdo 4:2; Ufu 20:5, 6. 3:12 1 Tim 6:12; Mdo 9:6. 3:14 1 Kor 9:24. 3:15 1 Kor 2:6. 3:16 Gal 6:16. 3:17 1 Kor 11:1; 1 Tes 1:7; 1 Pet 5:3. 3:18 1 Kor 1:23; Gal 6:12. 3:19 Rom 16:18. 3:20 Efe 2:6; Kol 3:1; Ebr 12:22. 3:21 1 Kor 15:43, 49, 53.

4:1 2 Kor 1:14; 1 Tes 2:19, 20. 4:3 Zab 69:28; Lk 10:20.

ninakusihi wewe vilevile, mutumishi mwenzangu wa kweli, saidia wanawake
hawa, kwa sababu walijitaabisha sana pamoja nami kwa Habari Njema, pa-
moja na Klementi vilevile, na wale wengine waliotenda kazi pamoja nami,
walio na majina yao katika kitabu cha uzima.

Furaha katika Kristo

4 Furahini katika Bwana siku zote; tena ninasema, Furahini. 5 Upole wenu
ujulikane na watu wote. Bwana ni karibu. 6 Musijisumbushe wenyewe kwa
neno lo lote; lakini katika kila neno kwa kuomba na kusihi pamoja na kushu-
kuru maombi yenu yajulikane na Mungu. 7 Na salama ya Mungu, inayopita
akili zote, italinda mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.

Mufikili maneno mazuri

8 Kwa kumaliza, ndugu zangu, maneno yo yote yaliyo ya kweli, maneno yo
yote yaliyo ya heshima, maneno yo yote yaliyo haki, maneno yo yote yaliyo
safi, maneno yo yote yenye kupendeza, maneno yo yote yenye sifa njema; uki-
wa wema wo wote na ikiwa sifa yo yote, fikilieni maneno haya. 9 Fanyeni ma-
neno muliyojifundisha na kuyapokea na kuyasikia na kuyaona ndani yangu, na
Mungu wa salama atakuwa pamoja nanyi.

Katika Kristo yote yanawezekana

10 Lakini ninafurahi sana katika Bwana kwa sababu sasa mwisho mumeni-
fikili tena; kama vilevile mulivyokuwa mukifikili hali yangu, lakini mulikosa
nafasi. 11 Si kwamba ninasema maneno haya kwa kuwa nina mahitaji; maana
nimejifundisha mwenyewe, kufurahi katika hali yo yote niliyo nayo. 12 Ninajua
kunyenyekezwa, na ninajua namna gani kuzidi; katika hali yo yote, na katika
maneno yo yote nimejifundisha kushiba na kuona njaa, kuwa na vitu vingi na ku-
pungukiwa. 13 Ninaweza kufanya maneno yote katika Kristo anayenitia nguvu.
14 Lakini mulifanya vema kushiriki pamoja nami katika taabu yangu. 15 Nanyi
wenyewe munajua, ninyi Wafilipi, ya kuwa katika mwanzo wa Habari Njema,
wakati nilipoondoka katika Makedonia, hakuna kanisa lingine lililoshirikiana
nami katika maneno ya kutoa na kupokea, ila ninyi peke yenu. 16 Kwa kuwa
hata kule Tesalonika mulituma kusaidia mahitaji yangu wakati na wakati. 17 Si
kwamba ninatamani zawadi; lakini ninatamani matunda yanayozidi kuwa
mengi katika hesabu yenu. 18 Lakini nina vitu vyote na kuzidi; nimejaa tele
nikiwa nimepokea kwa mukono wa Epafrodito vitu vilivyotoka kwenu, harufu
ya manukato, zabihu ya kukubaliwa inayopendeza Mungu. 19 Na Mungu
wangu atajaza mahitaji yenu yote kwa kadiri ya utajiri wake katika utukufu,
ndani ya Kristo Yesu. 20 Sasa kwa Mungu Baba yetu uwe utukufu kwa milele
na milele. Amina.

21 Musalimu kila mutakatifu katika Kristo Yesu. Ndugu walio pamoja nami
wanawasalimu ninyi. 22 Watakatifu wote wanawasalimu ninyi, zaidi wale walio
nyumbani mwa Kaisari.

23 Neema ya Bwana Yesu Kristo iwe pamoja na roho zenu.

4:4 Flp 3:1; 2 Kor 13:11. 4:5 Ebr 10:37; Yak 5:8, 9. 4:6 Mt 6:25–34; Kol 4:2; 1 Pet 5:7; Zab 145:18; Yn 14:27. 4:7 Kol 3:15. 4:8 Rom 12:17. 4:9 1 Tes 5:23; Rom 16:20; 1 Kor 14:33. 4:11 1 Tim 6:6. 4:12 2 Kor 6:10. 4:13 2 Kor 12:10; 2 Tim 4:17. 4:15 2 Kor 11:9. 4:17 1 Kor 9:11. 4:18 Kut 29:18; Eze 20:41; Flp 2:25. 4:22 Flp 1:13.

BARUA YA PAULO MUTUME
KWA

WAKOLOSAYI

1 Paulo, mutume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu, na Timoteo
ndugu yetu, 2 kwa watakatifu na ndugu waaminifu katika Kristo walio
katika Kolosayi: Neema iwe kwenu na salama toka Mungu Baba yetu.

Kazi ya Habari Njema

3 Tunashukuru Mungu, Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo, tukiwaombea
ninyi siku zote, 4 tukiwa tumesikia habari za imani yenu katika Kristo Yesu,
na za mapendo muliyo nayo kwa watakatifu wote, 5 kwa sababu ya tumaini
mulilowekewa akiba mbinguni, habari zake mulizosikia zamani katika neno la
kweli ya Habari Njema, 6 iliyofika kwenu; kama ni vile katika ulimwengu wote
ikizaa matunda na kukua kama inavyokua ndani yenu vilevile, tangu siku
muliposikia na kujua neema ya Mungu katika kweli; 7 kama vile mulivyofu-
ndishwa na Epafra, mujoli wetu mupenzi, aliye mutumishi mwaminifu wa
Kristo kwa ajili yetu, 8 aliyetuambia vilevile habari za mapendo yenu katika
Roho.

Kazi ya Kristo

9 Kwa sababu hii sisi vilevile, tangu siku tuliposikia, hatuachi kuomba na
kuwaombea ninyi, ili mujazwe kujua kwa mapenzi yake katika hekima yote
na ufahamu wa roho, 10 mutembee kama inavyostahili na Bwana kwa kumu-
pendeza kabisa, mukizaa matunda katika kila kazi njema, na kuzidi katika
kujua Mungu; 11 mukiwezeshwa kwa uwezo wote, kwa kadiri ya nguvu ya
utukufu wake, mupate kuwa na saburi yote na uvumilivu pamoja na furaha;
12 mukishukuru Baba aliyetustahilisha kupokea sehemu ya uriti wa watakatifu
katika nuru. 13 Naye alitutoa katika uwezo wa giza, akatuhamisha na kutui-
ngiza katika ufalme wa Mwana wa mapendo yake; 14 ndani yake tuna wokovu
wetu, usamehe wa zambi zetu. 15 Naye ni mufano wa Mungu asiyeonekana,
muzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. 16 Kwa kuwa katika yeye vitu vyote
viliumbwa vilivyo mbinguni na vilivyo duniani, vitu vinavyoonekana na visi-
vyoonekana, ikiwa ni viti vya wafalme ao usultani ao falme ao mamlaka;
vitu vyote viliumbwa kwa njia yake na kwa ajili yake. 17 Naye ni mbele ya
vitu vyote na ndani yake vitu vyote vinashikamana. 18 Naye ni kichwa cha
mwili, ulio kanisa; aliye mwanzo, muzaliwa wa kwanza kutoka katika wafu;
ili apate kuwa wa kwanza katika yote. 19 Kwa kuwa katika yeye ilipendeza
utimilifu wote ukae; 20 na kwa yeye kupatanisha vitu vyote kwake, akiwa
amefanya salama kwa njia ya damu ya musalaba wake; kwa yeye, kama ni vitu
duniani ao vitu mbinguni. 21 Nanyi, muliotengwa mbali zamani na mulikuwa
adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha ninyi sasa
22 katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake, ili awalete ninyi mbele yake,

1:1 Efe 1:1. 1:2 Rom 1:7; Efe 1:2. 1:3 1 Kor 13:13; Efe 1:16; 1 Tes 1:2, 3. 1:4 Efe 1:15. 1:5 1 Pet 1:4; Efe 1:13, 18. 1:6 1 Tim 3:16; Efe 1:13. 1:7 Kol 4:12. 1:9 Efe 1:8, 9, 15–17; Flp 1:9. 1:10 Efe 1:17; 2:10; 4:1; Flp 1:27. 1:11 1 Kor 1:5; Efe 1:18, 19; 3:16. 1:12 Efe 1:11, 18. 1:13 Kol 2:15; Lk 22:53; Efe 2:2; 6:12; 1:6. 1:14 Efe 1:7. 1:15 Ebr 1:3; 2 Kor 4:4; 1 Tim 6:16; Yn 1:18. 1:16 Yn 1:3, 10; Efe 1:10, 21. 1:17 Mez 8:25–27; Efe 1:22. 1:18 Efe 1:22; 4:15; 5:23; Mdo 4:2; 26:23; Ufu 1:5. 1:19 Efe 1:23; Kol 2:9; Yn 1:16. 1:20 Efe 1:7, 10; 2:13; 1 Yn 2:2. 1:21 Efe 2:1, 12; 4:18; Rom 5:10. 1:22 Efe 2:11, 14, 16; 5:27.

watakatifu na pasipo kilema, wala laumu; 23 kama mukidumu katika imani,
mukiwekwa juu ya musingi na kusimama imara, wala hamugeuzwi mbali na
tumaini la Habari Njema muliyosikia, iliyohubiriwa katika viumbe vyote chini
ya mbingu; nami Paulo nilifanywa mutumishi wake.

Siri ya Kristo ndani ya watu wake

24 Basi sasa ninafurahi katika mateso yangu kwa ajili yenu, na ninatimiza
katika mwili wangu yale yaliyokosa ya mateso ya Kristo kwa ajili ya mwili
wake, ndio kanisa lake. 25 Nami nimefanywa mutumishi wake, sawasawa na
uwakili wa Mungu niliopewa kwa faida yenu, nitimize Neno la Mungu, 26 siri
iliyofichwa tangu nyakati na vizazi vyote; lakini sasa imefunuliwa kwa wata-
katifu wake, 27 kwao Mungu alipendezwa kuwafunulia utajiri wa utukufu wa
siri hii katika Mataifa, iliyo Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu; 28 tuna-
yemuhubiri, tukionya kila mutu na kufundisha kila mutu na akili yote, ili
tupate kuleta kila mutu mutimilifu katika Kristo. 29 Kwa sababu hii ninaji-
taabisha, nikishindana na nguvu kwa kadiri ya kutenda kazi kwake anayetenda
kazi ndani yangu kwa nguvu.

Maonyo

2 Maana ninataka mujue ya kuwa ninashindana na nguvu sana kwa ajili
yenu, na kwa ajili ya wale wa Laodikia, na kwa ajili ya wote wasioona uso
wangu katika mwili; 2 ili mioyo yao ifarijiwe, wakiunganishwa pamoja katika
mapendo, wapate utajiri wote wa kufahamu kwa hakika, wapate kujua siri ya
Mungu, ndiye Kristo, 3 ndani yake hazina zote za hekima na kujua zinafichwa.
4 Ninasema maneno haya, hata mutu asiwadanganye ninyi na maneno ya kusha-
wishi. 5 Maana hata nikiwa mbali katika mwili, mimi ni pamoja nanyi katika
roho, nikifurahi na kutazama utaratibu wenu na uaminifu wa imani yenu katika
Kristo.

Tohara ya kweli

6 Basi kama mulivyopokea Kristo Yesu Bwana, mutembee vivyo hivyo ndani
yake, 7 mukiwekwa juu ya musingi na kujengwa ndani yake, na kusimamishwa
katika imani yenu, kama mulivyofundishwa vilevile, mukizidi kutoa kushu-
kuru.

8 Angalieni hata mutu asiwatege ninyi kwa elimu yake ya bule na madanga-
nyifu yake matupu, kwa desturi ya watu, kwa maneno ya ulimwengu, wala si
kwa Kristo. 9 Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa mwili.
10 Na ninyi mumetimilika katika yeye aliye kichwa cha falme zote na mamlaka.
11 Katika yeye mulitahiriwa vilevile kwa tohara isiyofanyika kwa mikono, kwa
kuondosha mwili wa nyama, kwa tohara ya Kristo, 12 mukizikwa pamoja naye
katika ubatizo, na katika huu mulifufuliwa pamoja naye kwa kuamini nguvu za
Mungu, aliyemufufua toka wafu. 13 Nanyi muliokuwa wafu kwa sababu ya
makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, ninyi aliwafanya hai pamoja
naye, akiwa ametusamehe makosa yetu yote; 14 akikwisha kuzima hati ile
iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu;

1:23 Mk 16:15; 1 Tim 3:16; Efe 3:17; Ebr 3:14. 1:24 Efe 3:1, 13. 1:25 Efe 3:2, 7, 8. 1:26 Rom 16:25, 26; Efe 3:3, 5, 9, 10. 1:27 1 Tim 1:1; Rom 16:25; Efe 3:9; 1:18. 1:28 Efe 4:13. 1:29 Flp 4:13; Efe 3:7, 20.

2:2 Kol 1:26; Efe 3:18. 2:3 Isa 45:3; Mez 2:3, 4; Efe 3:19; 1 Kor 1:24, 30. 2:4 Rom 16:18; Efe 4:17; 5:6. 2:5 1 Kor 5:3; 14:40. 2:6 Efe 4:17. 2:7 Efe 3:17; 2:20, 22. 2:8 Efe 5:6. 2:9 Yn 1:14, 16. 2:10 Efe 1:21. 2:11 1 Pet 3:21; Rom 2:29. 2:12 Kol 3:1; Rom 6:4; Efe 1:19, 20. 2:13 Efe 2:1, 5. 2:14 Efe 2:14, 15; 1 Pet 2:24.

akaiondosha na kuifunga kwa musalaba na misumari. 15 Akikwisha kuondosha falme na mamlaka akazionyesha waziwazi akizishangilia katika musalaba huu.

Kivuli cha mambo yanayokuja

16 Basi mutu asiwahukumu ninyi katika vyakula ao vinywaji ao kwa sababu ya siku kubwa, ao mwezi mwandamo ao siku ya sabato. 17 Mambo haya ni kivuli cha maneno ya kuja; lakini mwili ni wa Kristo. 18 Mutu asiwanyanganye ninyi zawabu yenu kwa kunyenyekea kwa mapenzi yake mwenyewe, na kuabudu malaika, akijitia katika maono yake na kujivuna bule kwa akili zake za mwili, 19 asiyeshika kichwa, kwa yeye mwili wote ukisaidiwa na kuunganishwa pamoja kwa viungo na mishipa, unakua kwa maongezo ya Mungu.

20 Basi ikiwa mumekufa pamoja na Kristo kwa maneno ya ulimwengu, kwa nini munajitia chini ya amri, kama wenye kuishi duniani, 21 musishike, musionje, musiguse, 22 (maneno haya yote yanaharibika wakati wa kutumiwa), mukifuata maagizo na mafundisho ya watu? 23 Maneno haya yanaonekana ya kwamba yana hekima katika kuabudu kwa mapenzi yao wenyewe, na katika unyenyekevu, na katika kutawala mwili kwa ukali; lakini hayafai kitu kwa kuzuiza tamaa za mwili.

Maisha mapya katika Kristo

3 Basi mukiwa mumefufuliwa pamoja na Kristo, tafuteni maneno yaliyo juu, pahali Kristo yuko, akiketi mukono wa kuume wa Mungu. 2 Tieni mafikili yenu juu ya maneno ya juu, wala si juu ya maneno yaliyo duniani. 3 Kwa maana mulikufa, na maisha yenu yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. 4 Wakati Kristo, aliye uzima wetu atakapofunuliwa, ninyi vilevile mutafunuliwa pamoja naye katika utukufu.

5 Basi ueni viungo vyenu vilivyo duniani; uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mafikili mabaya, na kutamani ndiyo kuabudu sanamu. 6 Kwa ajili ya maneno haya gazabu ya Mungu inakuja juu ya wana wa kuasi. 7 Katika haya ninyi mulitembea vilevile zamani, wakati mulipoishi katika maneno haya. 8 Lakini sasa ondosheni maneno haya yote: kasirani, hasira, uovu, matukano, na masemo ya haya vinywani mwenu. 9 Musiambiane uwongo, kwa kuwa mumeondosha kabisa mutu wa zamani na matendo yake, 10 na mumevaa mutu mupya anayefanywa mupya apate ufahamu sawasawa na mufano wake yeye aliyemwumba. 11 Hapa hapana Muyunani wala Muyuda, kutahiriwa wala kutokutahiriwa, mugeni wala mushenzi, mutumwa wala aliye huru; lakini Kristo ni yote, na katika yote.

12 Basi, mukiwa wachaguliwa wa Mungu, watakatifu na wapendwa, vaeni moyo wa rehema, wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu; 13 mukichukuliana na kusameheana kama mutu akiwa na sababu ya kushitaki mwenzake, kama vile Bwana alivyowasamehe ninyi, ninyi mufanye vivyo hivyo. 14 Na zaidi ya maneno haya yote muvae mapendo yaliyo kifungo cha utimilifu. 15 Na salama ya Kristo itawale mioyoni mwenu, kwa sababu yake muliitwa katika mwili mumoja; tena muwe watu wa kushukuru. 16 Neno la Kristo likae kwa wingi ndani yenu kwa hekima yote, mukifundishana na kuonyana kwa zaburi na nyimbo na tenzi za

2:15 Kol 1:13. 2:16 Rom 14:1–12. 2:17 Ebr 8:5; 10:1. 2:19 Efe 2:21; 4:15, 16. 2:20 Gal 4:3, 9. 2:21 Gal 6:8. 2:22 Isa 20:13; Mt 15:9. 2:23 Rom 13:14; 1 Tim 4:3.

3:1 Zab 110:1; Kol 2:12. 3:2 Mt 6:33. 3:3 Rom 6:2. 3:4 1 Kor 15:43; Flp 1:21; Gal 2:20. 3:5 Rom 6:6; 8:13; Efe 4:19; 5:3, 5. 3:6 Efe 5:6. 3:8 Efe 4:25–31; 5:4. 3:9 Efe 4:22. 3:10 Efe 4:24; Mwa 1:27. 3:11 Gal 3:28. 3:12 1 Pet 2:9; Efe 4:2, 32; 5:2. 3:13 Mt 6:14; Efe 4:32; 5:2. 3:14 Rom 13:8, 10; Efe 4:3. 3:15 Efe 4:4; Flp 4:7; 1 Kor 12:13, 37. 3:16 Efe 5:19.

roho, mukiimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu. 17 Na kila kitu munachofanya, katika neno ao katika tendo, fanyeni yote kwa jina la Bwana Yesu, mukishukuru Mungu Baba kwa yeye.

Maonyo kwa wote

18 Wake, mutii waume wenu kama inavyopendeza katika Bwana. 19 Waume, mupende wake wenu, wala musiwe na uchungu nao. 20 Watoto, mutii wazazi wenu katika maneno yote, maana neno hili linapendeza katika Bwana. 21 Baba, musichokoze watoto wenu, wasichoke katika roho zao. 22 Watumwa, mutii wale walio bwana wenu kwa maneno ya mwili katika maneno yote; si kwa utumwa wa macho kwa kupendeza watu, lakini na roho moja mukiogopa Bwana. 23 Kila kitu munachofanya, mukifanye kwa moyo, kama kwa Bwana, wala si kwa watu; 24 mukijua ya kuwa mutapokea kwa Bwana zawabu ya uriti; munatumikia Bwana Kristo. 25 Maana anayetenda mabaya atapata tena kwa mabaya aliyoyatenda; wala hakuna upendeleo.

4 Ninyi bwana, muwape watumwa wenu yaliyo haki na sawa; mukijua ya kuwa ninyi vilevile muna Bwana mbinguni.

Mashauri mema

2 Mudumu sana katika maombi, mukiangalia ndani yao pamoja na kushukuru; 3 mukituombea sisi vilevile, ili Mungu atufungulie mulango kwa neno lake, tuseme siri ya Kristo, kwa ajili yake nimefungwa; 4 ili niionyeshe, kama ninavyopaswa kusema. 5 Tembeeni kwa hekima mbele yao walio inje, mukikomboa wakati. 6 Masemo yenu yote yawe na neema siku zote, yakitengenezwa na chumvi, mupate kujua namna inavyowapasa ninyi kujibu kila mutu.

7 Tikiko, ndugu mupendwa na mutumishi mwaminifu na mujoli wangu katika Bwana, atawajulisha ninyi maneno yangu yote; 8 niliyemutuma kwenu kwa sababu hii tu mupate kujua hali yetu, naye afariji mioyo yenu; 9 pamoja na Onesimo, ndugu mwaminifu na mupendwa, aliye mutu wa kwenu. Wao watawajulisha ninyi maneno yote ya hapa kwetu.

Salamu

10 Aristarko aliyefungwa pamoja nami anawasalimu ninyi, na Marko, mujomba wa Barnaba (juu yake mumepokea maagizo: kama akifika kwenu, mumupokee), 11 na Yesu anayeitwa Yusto, walio watu wa tohara. Wao tu ni watenda kazi pamoja nami kwa ajili ya ufalme wa Mungu, watu walionifariji. 12 Epafra aliye mutu wa kwenu, mutumishi wa Kristo Yesu, anawasalimu ninyi, akifanya bidii siku zote kwa ajili yenu katika maombi yake, ili musimame wenye kutimia na kujua sana mapenzi yote ya Mungu. 13 Maana ninamushuhudia kwamba anajitaabisha sana kwa ajili yenu na kwa ajili yao walio katika Laodikia, na kwa ajili yao walio katika Hierapoli. 14 Luka, muganga mupendwa, na Dema wanawasalimu ninyi. 15 Salimuni ndugu walio katika Laodikia, na Nimfa, na kanisa lililo katika nyumba yake. 16 Na wakati barua hii itakapokwisha kusomwa katikati yenu, fanyeni isomwe katika kanisa la Laodikia

3:17 1 Kor 10:31; Efe 5:20. 3:18 Efe 5:22–6:9. 3:19 1 Pet 3:7. 3:25 Rom 2:11.

4:1 Law 25:43, 53. 4:2 1 Tes 5:17; Efe 6:18; Flp 4:6. 4:3 Rom 15:30; Efe 6:18, 19; 2 Tes 3:1; 1 Kor 16:9. 4:4 Efe 6:20. 4:5 Efe 5:15, 16; 1 Tes 4:12. 4:6 Efe 4:29; Mk 9:50; 1 Pet 3:15. 4:7 Efe 6:21. 4:8 Efe 6:22. 4:9 Flm 1:10. 4:10 Mdo 19:29; 27:2; 18:27. 4:12 Kol 1:7. 4:14 2 Tim 4:10, 11; Flp 1:24.

vilevile; nanyi vilevile musome barua toka Laodikia. 17 Mumwambie Arkipo: Angalia sana kwa utumishi uliopewa na Bwana, ili uutimize.

18 Salamu yangu mimi Paulo na mukono wangu mwenyewe. Kumbukeni vifungo vyangu. Neema iwe pamoja nanyi.

BARUA YA KWANZA YA PAULO MUTUME KWA

WATESALONIKA

Kazi ya imani, taabu ya mapendo, saburi ya tumaini

1 Paulo, na Silvano, na Timoteo, kwa kanisa la Watesalonika katika Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo: Neema iwe kwenu na salama toka Mungu Baba yetu, na Bwana Yesu Kristo.

2 Tunashukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu ninyi wote, tukiwataja ninyi katika maombi yetu; 3 tukikumbuka pasipo kuacha kazi yenu ya imani, na taabu yenu ya mapendo, na saburi yenu ya tumaini katika Bwana wetu Yesu Kristo, mbele ya Mungu Baba yetu; 4 tukijua, ndugu munaopendwa na Mungu, kuchaguliwa kwenu, 5 sababu Habari Njema yetu haikufika kwenu katika neno tu, lakini vilevile katika uwezo na katika Roho Mutakatifu, na katika matumaini mengi; sawasawa munavyojua tulikuwa watu wa namna gani katikati yenu kwa ajili yenu. 6 Mukakuwa wafuataji wetu, na wafuataji wa Bwana, mukikwisha kupokea neno katika mateso mengi, pamoja na furaha ya Roho Mutakatifu; 7 hata mulikuwa mufano kwa watu wote wanaoamini katika Makedonia na Akaya. 8 Sababu sauti ya neno la Bwana ilitoka kwenu, si katika Makedonia na Akaya tu, lakini katika kila pahali imani yenu kwa Mungu imetangazwa; hata hatuhitaji kusema neno. 9 Kwa sababu wao wenyewe wanatangaza habari zetu namna tulivyoingia katikati yenu; na namna gani mulivyogeuka kwa Mungu toka sanamu, kutumikia Mungu aliye hai, na Mungu wa kweli; 10 na kungojea Mwana wake kutoka mbingu, aliyemufufua toka wafu, hata Yesu, mwenye kutuokoa toka gazabu itakayokuja.

Mutumishi mwema na zawadi yake

2 Kwa maana ninyi wenyewe, ndugu, munajua ya kama kuingia kwetu kwenu hakukuwa bule: 2 lakini tukikwisha kuteswa mbele na kutendwa jeuri, kama munavyojua, katika Filipi, tulikuwa na uhodari katika Mungu wetu kuwaambia ninyi Habari Njema ya Mungu katika kuishindania sana. 3 Kwa maana maonyo yetu si ya ukosefu, wala ya uchafu, wala ya hila: 4 lakini kama tulivyokubaliwa na Mungu kuaminiwa na Habari Njema, hivi tunavyosema; si kwa kupendeza watu lakini kwa kupendeza Mungu anayepima mioyo yetu. 5 Sababu hatukuwa na maneno ya kujipendekeza wakati wo wote, kama munavyojua, wala maneno ya juujuu ya kuficha choyo, Mungu ni mushuhuda;

4:17 Flm 1:2. 4:18 1 Kor 16:21; 2 Tes 3:17.

1:1 Mdo 15:40; 17:1; 2 Tes 1:1. 1:2 2 Tes 1:11. 1:3 1 Kor 13:13; Kol 1:4, 5. 1:5 1 Kor 2:5. 1:6 1 Kor 4:16; Mdo 13:52; 2 Tes 3:9. 1:7 1 Tes 4:10; Flp 3:7; 1 Pet 5:3. 1:8 Rom 1:8. 1:9 Mdo 14:15; Yn 17:3; 1 Kor 12:2. 1:10 1 Tes 5:9; Tit 2:13; Mdo 17:31.

2:1 1 Tes 1:5, 9; 2 Tes 3:7. 2:2 Mdo 16:20–24; 17:1–5. 2:4 Yer 11:20; Gal 1:10; 1 Tim 1:11. 2:5 Mdo 20:33; Mk 12:40; 2 Pet 2:3.

6 wala hatukutafuta sifa ya watu, wala kwenu, wala kwa wengine, wakati tulipoweza kuwa na amri kama mitume ya Kristo. 7 Lakini tulikuwa wapole katikati yenu kama mulezi anayetunza watoto wake mwenyewe; 8 hata hivi, tukiwa na hamu sana kwenu, tuliona furaha kuwapa ninyi, si Habari Njema ya Mungu tu, lakini roho zetu wenyewe vilevile, kwa sababu mumekuwa wapenzi wetu. 9 Sababu munakumbuka, ndugu, taabu yetu na kazi yetu: tukitumika usiku na muchana ili tusilemee mutu ye yote kwenu, tukawahubiri ninyi Habari Njema ya Mungu. 10 Ninyi ni washuhuda, na Mungu vilevile, namna tulivyokaa katikati yenu ninyi wenye kuamini; kwa utakatifu na kwa haki, pasipo laumu: 11 kama munavyojua namna tulivyoonya kila mumoja wenu, kama baba anavyoonya watoto wake mwenyewe, tukiwasibitisha ninyi, na kushuhudia, 12 ili mutembee mwenendo kama inavyofaa kwa Mungu, mwenye kuwaita ninyi mwingie ufalme wake na utukufu wake.

13 Kwa sababu hii sisi tunashukuru Mungu pasipo kuacha, sababu wakati mulipopokea Neno la Mungu mulilosikia kwetu, mulilipokea si kama neno la watu, lakini, kama lilivyo kweli Neno la Mungu, linalotenda kazi vile ndani yenu munaoamini. 14 Maana ninyi, ndugu, mulikuwa wafuataji wa makanisa ya Mungu yaliyo katika Yudea, katika Kristo Yesu: kwa sababu ninyi vilevile mulipata mateso yale yale kwa watu wa taifa lenu wenyewe, waliyoyapata kwa Wayuda; 15 walioua Bwana Yesu, na manabii, na kututukuza sisi, wala hawapendezi Mungu, wala hawapatani na watu wote; 16 wakitukataza sisi kusema na Mataifa wapate kuokolewa; ili kutimiza zambi zao siku zote: lakini gazabu imewafikia hata mwisho.

17 Lakini sisi, ndugu, tukitengana nanyi kwa saa kidogo, kwa uso si kwa moyo, tulijaribu sana kuona nyuso zenu kwa hamu kubwa: 18 kwa hivi tulitaka kuja kwenu, mimi Paulo, mara ya kwanza na mara ya pili: lakini Shetani alituzuiza. 19 Maana tumaini letu, ao furaha yetu, ao taji yetu ya kujisifu ni nini? Si ninyi, mbele ya Bwana wetu Yesu wakati wa kuja kwake? 20 Maana ninyi ni utukufu wetu na furaha yetu.

Utakaso wa Wakristo

3 Kwa sababu hii, wakati tusipoweza kuvumilia tena, tuliona vema kuachwa katika Atene peke yetu; 2 tukatuma Timoteo, ndugu yetu na mutumishi wa Mungu katika Habari Njema ya Kristo, kuwasimamisha ninyi, na kuwafariji ninyi kwa habari za imani yenu: 3 mutu asifazaishwe na mateso haya; maana ninyi wenyewe munajua ya kwamba tumewekwa kwa maneno haya. 4 Kwa maana wakati tulipokuwa kwenu, tuliwaambia ninyi mbele ya kuwa tutapata mateso; kama ilivyotokea, nanyi munajua. 5 Kwa sababu hii mimi, wakati nilipokuwa siwezi kuvumilia tena, nilituma mutu nipate kujua imani yenu, asiye mujaribu akawajaribu ninyi, na taabu yetu ikakuwa pasipo faida. 6 Lakini wakati Timoteo alipokuja kwetu sasa toka kwenu, alituletea sisi habari njema za imani yenu na mapendo yenu, na ya kwamba munatukumbuka vema siku zote, mukitamani kutuona sisi, kama sisi kuwaona ninyi; 7 kwa sababu hii, ndugu, tulifarijiwa kwa habari zenu katika taabu yetu yote na mateso yetu kwa sababu ya imani yenu; 8 kwa maana sasa tunaishi kama mukisimama imara katika Bwana. 9 Maana mashukuru gani tunayoweza kulipa Mungu tena kwa

2:6 Yn 5:41, 44. 2:9 1 Kor 4:12; Mdo 20:34. 2:11 Mdo 20:31. 2:12 Efe 4:1; Flp 1:27; 2 Tes 1:5; 1 Pet 5:10. 2:13 1 Tes 1:2; Gal 1:11; 2 Tes 2:13. 2:15 Mdo 2:23; 7:52. 2:16 Mwa 15:16; Mt 23:32, 33. 2:17 Rom 1:11, 13. 2:19 Flp 2:16; 4:1; 2 Tes 1:4.

3:1 Mdo 17:14, 15. 3:2 Mdo 16:1–3. 3:3 Efe 3:13; 2 Tim 3:12; 2 Tes 1:4. 3:4 2 Tes 3:10; Mdo 14:22. 3:5 Flp 2:16. 3:6 Mdo 18:5. 3:7 2 Tes 1:4.